**Zitto** na Mbatia wataka kuteta na serikali kisa Mbowe

UKURASA 5



**Spika** atetea tozo miamala ya simu kwa hoja moja

UKURASA 2




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Julai 24, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580651

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## BAA LA CORONA

# Hali ni mbaya

**•WAZIRI** akiri maambukizi juu kisa ulegevu, KCMC yazidiwa, chanjo kitaifa rasmi leo....

*Endelea ukurasa 3 & 5*




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mwenendo wa corona nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Machinga naye adai kuporwa 35,000/- na Sabaya

UKURASA 4

## Lissu atoa msimamo tuhuma kina Mbowe

UKURASA 2



Tundu Lissu

**MICHEZO** **GOMES: TUMEKUJA KUFUNGA HESABU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Spika Ndugai atetea tozo miamala ya simu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job ndugai, amelizungumzia sakata la tozo za miamala ya simu, akiwataka wanaolalamika kuja na njia mbadala ya namna serikali itakavyopata fedha ili kutekeleza miradi ya maendeleo.

Ndugai alitoa kauli hiyo jana katika kikao cha viongozi wa Mkoa wa Dodoma kilicholenga kutathimini utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema wabunge waliamua kupitisha suala hilo la tozo za miamala kwa kuwa fedha inayopatikana katika eneo hilo ni nyingi na itaisaidia serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Fedha itakayopatikana inakwenda katika mfuko maalum na zinakwenda kuwasaidia wananchi kupata huduma muhimu zikiwamo umeme, maji, kujenga madarasa, madaraja, kupitia tozo tulizopitisha.

"Ndiyo mana sisi wabunge tukaamua kwenda kwenye suala la muamala kwa sababu tuna uhakika fedha itakayopatikana itasaidia katika miradi ya maendeleo.

"Tumepitisha sisi, tukatunga sheria sisi, tunataka kuliona hilo, hakuna njia ya mkato, sasa wewe ambaye unapinga tupe njia mbadala, tutapata wapi fedha, tunafikaje 2025?

"Kwa hiyo maamuzi ni hayo tumeyafanya kwa nia njema kabisa, kwamba 2025 tuwe tumetoka, tuwe ni taifa la Tanzania ambalo ni tofauti, Tanzania nzima," alisema Ndugai.

Akizungumzia kuhusu Mkoa wa Dodoma, aliwataka watendaji mkoani humo kujitathimini katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuwa serikali imekuwa ikitimiza wajibu wake kwa kuleta fedha kwa wakati lakini alidai tatizo lipo kwa watendaji.

"Nitolee mfano, Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, aliyetoka Simiyu kule alifanya kazi nzuri, hivyo hapa akishindwa kufanya vizuri tujue kabisa tatizo lipo kwetu," alisema.

Awali, akifungua kikao kazi hicho, Mtaka alitaja vipaumbele vinne ambavyo atavisimamia kwenye mkoa huo kuwa vinajumuisha elimu, utatuzi wa migogoro ya ardhi, kilimo na ufugaji na huduma bora za sekta za afya huku akitangaza alizeti kuwa zao la biashara la mkoani humo.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuwa timu katika kutekeleza mambo yanayohusu maendeleo.

"Ninawasihi tuwe na lugha ya pamoja, yapo mambo mazuri wenzetu wameyafanya, hivyo lazima tuyaendeleze, sisi Dodoma tuna utofauti, tunabeba haiba ya makao makuu ya nchi, hivyo ni lazima tuwe na matarajio makubwa," alisema Mtaka.

Kuhusu kiwango cha elimu, alisema Dodoma ina hali mbaya kwenye ngazi zote ikiwamo mitihani ya majaribio.

Pia aliagiza halmashauri zote nane za Dodoma kuwa na ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitauingizia mkoa fedha za kutosha kuendesha miradi mbalimbali. Pamoja na hayo, alisema anatamani kuona kaya zikipanda miti mingi kwa ajili ya utunzaji wa mazingira pamoja na kuweka mipango mizuri ya utunzaji wa mazingira.

"Watumishi waongo na wachonganishi siwapendi, watu wanaochonganisha watu, hasa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, tumekutanishwa na kazi, tufanye kazi tuheshimiane, kiongozi haongozwi," alisema.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhi zawadi ya mlango wa Zanzibar kwa mgeni wake Waziri Mkuu mstaafu wa Uingereza, Tony Blair, baada ya kumaliza mazungumzo yao, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Lissu atoa msimamo tuhuma kina Mbowe

**Na Romana Mallya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ametangaza msimamo wa chama hicho dhidi ya kukamatwa na kushikiliwa kwa viongozi wao, akiwamo Mwenyekiti, Freeman Mbowe.

Amesema licha ya Jeshi la Polisi kuwakamata na kuwashikilia viongozi wao hao, chama chao kinaendelea kudai Katiba Mpya na kuiarifu dunia kinachoendelea nchini.

Lissu alitangaza uamuzi huo jana ikiwa ni saa chache baada ya Jeshi la Polisi kutangaza linamshikilia Mbowe na watu wengine kadhaa, wakikabiliwa na tuhuma za kuratibu kundi la kigaidi na kupanga njama za kuua viongozi.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika kwa njia ya mtandao jana, Lissu ambaye kwa sasa anaishi Ubelgiji, alisema ataongoza kampeni hiyo ya kuiarifu dunia kinachoendelea Tanzania katika uga wa siasa.

Alisema Kamati Kuu ya CHADEMA imeazimia kuunda kamati ya ndani kwa ajili ya kuratibu shughuli zote za kampeni ya kutafuta Katiba Mpya na kuhakikisha wote aliodai walioonewa, wanapata msaada.

"Kumkamatamwenyekiti (Mbowe) haitatufanya turudi nyuma kudai Katiba Mpya, Kamati Kuu imeazimia jitihada za ndani na nje lazima ziendelee na mambo ya kudai Katiba Mpya," alisema.

Akijibu swali lililotaka kufahamu endapo Mbowe akishtakiwa kwa makosa hayo yasiyokuwa na dhamana na kwenda gerezani, atarejea nchini kukiendesha chama na mustakabali wa usalama wake, Lissu alisema CHADEMA ina viongozi wengi wakiwamo wa Kamati Kuu.

"Endapo mwenyekiti atashindwa kutekeleza wajibu wake kikamilifu kwa sababu ya kuwa gerezani, chama kitaendeshwa na viongozi watakokuwapo.

"Leo (jana) ninazungumza na ninyi nikiwa Ubelgiji na nyie mpo Dar es Salaam, lakini tunawasiliana vizuri. Jana (juzi) niliendesha kikao cha Kamati Kuu nikiwa Ubelgiji na wajumbe wakiwa mikoa mbalimbali na uamuzi umefanyika vizuri.

"Kwa sababu hiyo, yale yaliyokuwa hayawezekani zamani wakati hakuna njia za kisasa za mawasiliano, sasa yanawezekana," Lissu alitamba.

Alisisitiza kuwa hata akiendelea kuwapo Ubelgiji shughuli za CHADEMA na vikao vya chama vitaendelea kufanyika.

Kuhusu taarifa ya Jeshi la Polisi iliyotolewa juzi na Msemaji wake, David Misime, Lissu alisema taarifa hiyo ni rasmi na wanaifanyika kazi, huku akidai tayari wameshapata nakala za mashtaka.

"Tunafahamu, ukijulishwa mapema unachukua tahadhari mapema, tumejulishwa mapema kwamba wanatarajia kumshtaki mwenyekiti kwa ugaidi, tunachukua hatua mapema.

"Tunapiga kelele ili dunia ifahamu kinachokuja, ambacho wamesema wao wenyewe, waende mahakamani watakuta dunia nzima inawasubiri," alisema.

Alipoulizwa kama anafikiri kuichafua Tanzania kimataifa italeta suluhu ya matatizo, Lissu alivirushia lawama vyombo vya dola kwa kudai kuwa vinawafungulia kesi za uongo ambazo ndizo zinazochafua nchi na wao hawatafumbia macho, bali watatangaza dunia nzima.

Alipoulizwa kuhusu uhalali wa kupata misaada ya kifedha kutoka kwa nchi zinazounga mkono, Lissu alisema siyo kosa la jinai chama chao kupata msaada huo kutoka kwa nchi yoyote ikiwa una malengo halali.

"Ukweli ni kwamba hatujapata msaada huo bado, tunaomba watusaidie lakini bado hatujaupata," alisema.

Alipotakiwa kuweka wazi lini atarejea rasmi nchini, Lissu alisema kwa hali ilivyo, itabidi wafanye mawasiliano na viongozi ili kujua ni muda gani mzuri wa kurudi.

Kuhusu msimamo wa CHADEMA kutowawekea watu wake dhamana kuanzia sasa, Lissu alidai wamefikia hatua hiyo baada ya miaka mingi Jeshi la Polisi kuwapotezea muda mahakamani.

"Wanakukamata kwa makosa ya kutunga, wanakuweka ndani halafu unatumia miaka miwili au mitatu kuripoti kituo cha polisi, tumesema kuanzia sasa wafanye wanavyotaka.

"Kama wanataka kumshikilia mwenyekiti kwa mwaka mzima, wafanye, wanataka kumpeleka mahakamani wafanye, wanataka kumnyima dhamana, wafanye hivyo kama wanataka, hatutatoa ushirikiano kwa kukandamizwa kwa namna hii," alisema.

Lissu pia alisema kikao cha Baraza Kuu kilikuwa kimepangwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu na Kamati Kuu inatarajia kuketi leo ili kuzungumzia hatma ya kikao hicho.

## HABARI KITAIFA

# Majaliwa: Kero ya maji itaisha

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali imedhamiria kumaliza tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika vijiji vyote nchini ikiwamo Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi.

Amesema suala la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali, hivyo upatikanaji wa huduma hiyo ni endelevu.

"Tutaendelea kuboresha miradi ya maji ili maeneo yote nchini yapate maji ya uhakika," Majaliwa alisema wilayani Ruangwa jana kwenye mikutano ya hadhara iliyofanyika katika vijiji vya Mpara, Mtimbo, Mmawa, Chikoko, Chinokole na Kilimahewa.

Alisema serikali inatekeleza kampeni ya 'kumtua mama ndoo kichwani' ili kuhakikisha wananchi wote nchini wanapata huduma hiyo karibu na maeneo yao ya makazi.

Aliwaomba wananchi waendelee kuiamini serikali yao kwa sababu imedhamiria kuwatumikia.

Akizungumzia kuhusu tatizo la maji wilayani Ruangwa, Majaliwa alisema serikali inatekeleza ujenzi wa mradi wa maji wa Mbwinji ambao unatoa maji Ndanda hadi Ruangwa.

"Mradi huu mkubwa unatarajiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la upatikanaji wa maji wilayani Ruangwa," alisema.

Waziri Mkuu alisema mbali na huduma ya maji safi na salama, serikali pia imedhamiria kusambaza umeme katika vijiji vyote ambavyo bado havijaunganishiwa nishati hiyo nchini, hivyo akawataka wananchi wafanye maandalizi ya kufikisha nishati hiyo katika makazi yao.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inapata umeme kwa gharama nafuu na ametenga fedha nyingi zitakazotosheleza kusambaza umeme nchi nzima vikiwamo na vijiji vya ya Ruangwa. Gharama za kuunganishiwa umeme huo ni Sh. 27,000.

Waziri Mkuu alisema wananchi hawatowajibika tena katika kulipia gharama za nguzo wala fomu za maombi ya kuunganishiwa umeme kwa sababu tayari gharama hizo zote zimeshabebwa na serikali.




Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Ramadhani Mtindasi, kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji wilayani Kigamboni unaohusisha ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji lenye ukubwa wa lita milioni 15, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KCMC yazidiwa wagonjwa wahitaji mitungi Oksijeni

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC iliyoko Moshi mkoani Kilimanjaro, inakabiliwa na uhaba wa mitungi ya Oksijeni kutokana na kuwapo kwa idadi kubwa ya wagonjwa wa corona.

Imebainisha kuwa mgonjwa mmoja anatumia wastani wa mitungi 10 hadi 12 kwa siku.

Akizungumza na Nipashe jana hospitalini huko, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Profesa Gilleard Masenga, alisema wagonjwa wanaofikishwa hospitali huko kwa sasa hutumia mitungi zaidi ya 400 kwa siku.

"Wagonjwa wanakuja wakiwa katika hali mbaya na wengi wao ni wenye umri mkubwa, hutumia mitungi 10 hadi 12 kwa siku, tatizo ni kubwa, wananchi msichukulie mzaha, ni ugonjwa hatari, tuchukue tahadhari kulingana na maelekezo tunayopewa na Wizara ya Afya," alionya.

"Ni kweli tuna kiwanda hapa KCMC cha kuzalisha mitungi ya Oksijeni na uzalishaji wetu ni mitungi 400 kwa saa 24 na tulikiweka mwaka jana, tuliona hili litatusaidia kwa miaka 20 ijayo," alisema.

Prof. Masenga alisema matumizi yao kwa siku yalikuwa mitungi 50 hadi 60, lakini kuanzia mwaka jana, uhitaji uliongezeka kwa kasi hadi kufika sasa wanatumia mitungi 400 kwa siku.

Alisema ni mara chache kuwaona vijana wanalazwa hospitalini na kuhitaji huduma hiyo, hilo likiwapa ishara kwamba watu wenye umri mkubwa ndiyo wanakabiliwa na magonjwa.

Ofisa Afya Manispaa ya Moshi, Sebastien Mgeta, alisema bado mwitikio wa wananchi kuchukua hadhari dhidi ya corona ni mdogo.

"Kutokana na hali ya Uviko-19 ilivyo ndani ya jamii yetu, na mwitikio bado ni mdogo kwa wananchi, imetulazimu kutumia viongozi waliopo ndani ya jamii kutoa elimu ya namna bora ya kufuata mashati ya Wizara ya Afya," alisema.

Baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Moshi mkoani, akiwamo Lidya Mushi, waliiomba serikali kuingilia kati vyombo vya usafiri zikiwamo dalala na bajaji wanaojaza abiria kupitiliza. "Katika Stendi Kuu ya Mabasi Moshi watu wameacha utaratibu wa Wizara ya Afya, zipo daladala na Costa husimamisha watu jambo ambalo linaweza kuwa sehemu ya ongezeko la maambukizi," alisema Edmond Msofe.

Julai 22 mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai, alipiga marufuku mikusanyiko na kuagiza Jeshi la Polisi kuzuia mikusanyiko isiyo ya lazima ili kudhibiti maambukizi ya corona yanayoonekana kushika kasi kwa sasa nchini.

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**MIRAJI SAIDI DANDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **PIKIPIKI** yenye jina la **FRANK AUGUSTINO NGODA** aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 315 CHH**.Chasis **No. MD2A21BY5KWD86225**, Engine No. **PFZWKD58021** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/R-B/283942/2021.**

11631702

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.222/2021**

Ombi la **REHEMA RAJABU MADUKI** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **RAJABU MADUKI SOZI**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 23/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 20/07/2021**

116371502

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**TRY ANONI SANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA PASSO** yenye namba za usajili **T 718 DNN** ,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KAG/BUK/RB/864423/2021**

116372002

**MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD,** Madalali tajwa hapo chini tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za wadaiwa Sugu kama ilivyotangazwa kwenye gazeti/;-

| **Mdaiwa/ mdhamini** | **Dalali** | **Aina** ya **Mali** | **Tarehe ya mnada - Mahali** |
|---|---|---|---|
| Mwinyimvua Mtiga Lubawa /Samira Marcus Mgombele | **SEPCO** Debt Collection & Auctioneering Co. Ltd | Nyumba PLT No. 25 Block X | 30.07.2021 Magomeni - Mtaa Mwinyi mkuu-Dar |
| Irene Matiku Nyamtonga | **RAISSA** Company Ltd | Kiwanja | 30/07/2021 Kitongoji cha Bwilingu Chalinze-Pwani |
| Yahaya K Ally | **Diamond Credit Recovery** | Nyumba ambayo haijaisha | 06/08/2021 Mtaa wa Kiegea A Kihonda Morogoro |

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

Mawasiliano piga:
SEPCO - 0715683777/0712670704
RAISSA - 0757433333/0652113262
Diamond - 0746112953/0789455445

116372102

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**VENUS RIDHUAN MRINGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **DAIHATSU BEGO** yenye namba za usajili **T 439 DNZ** chasisi namba **J200G0000832**,engine namba **3SZ1539222**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/CEN/R-B/363357/2021**

11637l602

# Shahidi adai kuporwa 35,000/- na Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake wawili, wakiingia katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha jana, kusikiliza mashtaka ya kesi ya jinai yanayowamkabili. **PICHA: ALLAN ISACK**

SHAHIDI wa tatu wa Jamhuri, Ramadhani Rashid (26), amedai kuporwa Sh. 35,000 na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Rashid alipanda jana kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha kutoa ushahidi katika kesi inayomkabili Sabaya (34).

Kiongozi huyo pamoja na Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Katika ushahidi wake, Rashidi alidai mahakama uhalifu ulitendwa na washtakiwa hao, katika duka la Mohamed Saad, lililoko eneo la Soko Kuu, jijini Arusha.

Shahidi huyo, mkazi wa kona ya Esso, Kata ya Nganenaro, ni mfanyabiashara mdogo (machinga), ambaye anauza bidhaa mbalimbali zikiwamo vyandarua, mazulia, mashuka na mapazia.

Wakili wa Serikali, Baraka Mgaya, alimuhoji shahidi huyo kama ifuatavyo;-

**Swali:** Hebu ielezee mahakama Februari 9, mwaka huu, ulikuwa wapi na ulikuwa unafanya nini?

**Jibu:** Nakumbuka siku hiyo nilikuwa dukani kwangu ninapofanyia biashara yangu. Siku hiyo nilipata mteja lakini sikuwa na bidhaa ambayo alihitaji, hivyo nilimwomba anisubiri niende sehemu kumchukulia.

Niliondoka kwenda kuchukua bidhaa sehemu ninayochukulia nikakuta geti la duka la Shahid Store limefungwa. Nilijaribu kufungua geti kwa kuwa ni sehemu niliyoizoea na niliingia ndani na nilichukua bidhaa hiyo na kwenda kaunta kulipa fedha.

**Swali:** Nini kilitokea hapo dukani?

**Jibu:** Wakati nikiwa nimeshika bidhaa hiyo, alikuja mtu mmoja akaniuliza umefuata nini hapa?

**Swali:** Hao watu wawili na mmoja aliyekufuata walikuwa wa jinsia gani?

**Jibu:** Watu hao wawili walikuwa wa jinsia ya kiume.

**Swali:** Na ilikuwa mara yako ya ngapi kuwaona?

**Jibu:** Ilikuwa mara yangu ya kwanza kuwaona.

**Swali:** Baada ya kukuuliza umefuata nini dukani hapo nini kiliendelea?

**Jibu:** Nilipoangalia pembeni niliona watu wamewekwa chini ya ulinzi akiwamo yule anayepokea fedha dukani. Mimi niliwaambia nimekwenda hapo kuchukua bidhaa kwa kuwa ni machinga.

**Swali:** Nini kilifuata baada ya kuulizwa hivyo?

**Jibu:** Yule jamaa aliyeniuliza kuwa nimefuata nini dukani aliagiza nitolewe 'lock', nikaanza kupigwa vibao vya masikioni na usoni.

**Swali:** Baada ya kutolewa 'lock' nini kiliendelea?

**Jibu:** Waliendelea kunipiga na nilipiga kelele kumwita Mungu, huku wakipekua kwenye mifuko ya nguo yangu.

**Swali:** Ulipopigwa nini kiliendelea?

**Jibu:** Walinipekua mifukoni walichukua simu, fedha na karatasi ya vitu ambayo nilikuwa nimevifuata dukani.

**Swali:** Je, ilikuwa ni pesa kiasi gani zilizochukuliwa?

**Jibu:** Fedha iliyochukuliwa ni Sh. 35,000.

**Swali:** Ni simu gani iliyochukuliwa?

**Jibu:** Simu aina ya Tekno Pop1

**Swali:** Baada ya simu kuchukuliwa nini kiliendelea?

**Jibu:** Huyo jamaa aliagiza niwekwe chini ya ulinzi na kulala kwa tumbo kwenye sakafu.

**Swali:** Je, baada ya kuwekwa chini ya ulinzi nini kilitokea?

**Jibu:** Huyo jamaa alikuwa anazungumza na huyo mwenye duka.

**Swali:** Walikuwa wazungumzia nini?

**Jibu:** Huyo mwenye duka alikuwa anaulizwa na huyo jamaa kwa nini hawatoi risiti iliyokamilika wanapowauzia wateja bidhaa. Huyo mwenye duka alimjibu kwamba risiti wanatoa na alipokuwa akijibu waliendelea kumpiga.

Baada ya hapo huyo aliyekuwa akimhoji mwenye duka alikuwa akimlazimisha kuzungumza kile alichotaka yeye.

**Swali:** Ni jambo gani alitaka waseme?

**Jibu:** Alitaka mwenye duka kukubali kwamba hawatoi risiti wanapouza bidhaa na wakati mwingine ilibidi akubali kwa kuwa alipokataa waliendelea kumpiga sana.

**Swali:** Wakati tukio hilo likiendelea nini kilitokea?

**Jibu:** Jamaa alichukua simu ya mwenye duka kumrekodi kwamba wanafanya biashara bila ya kutoa risiti.

**Swali:** Kitu gani kingine kiliendelea?

**Jibu:** Huyo jamaa alimwambia huyo mwenye duka mbona mnafanya biashara ya kubadilisha dola.

**Swali:** Mwenye duka alijibu nini baada ya kuambiwa hivyo?

**Jibu:** Alimwambia huyo mtu kuwa hawafanyi biashara ya kubadilisha dola.

**Swali:** Wakati mkiwa chini ya ulinzi nini niliendelea?

**Jibu:** Huyo mtu alikuwa akimwambia aliyekuwa anauza dukani ampigie mwenye duka ili aende dukani kwa kuwa wanamhitaji.

**Swali:** Baada ya simu kupigwa huyo mwenye duka nini kilitokea?

**Jibu:** Mwenye duka hakuja yeye bali alikuwa ndugu yake anaitwa Hajirini.

**Swali:** Baada ya Hajirini kufika nini kilitokea?

**Jibu:** Hajirini alimsalimia huyo mtu kwa kumwambia Lengai Ole Sabaya heshima yako.

**Swali:** Huyo mtu alijibu nini baada ya kusalimiwa?

**Jibu:** Alimwuliza kama yeye ndiye Mohamed Saada.

**Swali:** Je huyo Hajirini alijibu nini?

**Jibu:** Alimwambia huyo mtu kuwa yeye si mhusika bali ni mdogo wake tu.

**Swali:** Baada ya hapo?

**Jibu:** Sabaya alimwambia Hajirini kuwa anamtaka mwenye duka.

**Swali:** Je, Hajirini alimjibu vipi huyo mtu?

**Jibu:** Alimwambia kuwa ndugu yake yuko mbali ndiyo sababu amemtuma kwa kuwa hawezi kufika dukani.

**Swali:** Baada ya Hajirini kuwaeleza kuwa ndugu yake hawezi kufika nini kiliendelea?

**Jibu:** Sabaya alimwambia kuwa wanafanya biashara kimakosa kwa kuwa hawatoi risiti na Hajirini alimwambia kwamba duka si lake bali ni muuzaji tu.

**Swali:** Baada ya Hajirini kusema hivyo nini kilitokea?

**Jibu:** Baada ya muda kidogo aliingia mtu mwingine akasalimia kwa kusema habari za saa hizi Mheshimiwa Lengai Ole Sabaya.

**Swali:** Je huyo mtu alijibiwa vipi?

**Jibu:** Sabaya alimwambia kuwa wewe ni Diwani wa Kata ya Sombetini ni kitu gani kimekuleta huku.

**Swali:**Alisalimia hivyo nini kilitokea?

**Jibu:** Diwani wa Sombetini alimjibu Sabaya kwa kumweleza "wewe ni Mkuu wa Wilaya wa Hai nini kimekuleta huku na alimwambia Arusha kuna Mkuu wa Wilaya na TRA wote wapo hapa wao ndio walitakiwa kushughulikia suala haya."

**Swali:** Baada ya majibu hayo nini kilifuata?

**Jibu:** Sabaya alisema Diwani huyo na yeye anashirikiana na watu hao, hivyo aliagiza atolewe "lock" yaani kupigwa.

**Swali:** Baada ya kumalizana na Bakari Msangi nini kiliendelea?

**Jibu:** Sabaya alituhurusu mimi na kijana mmoja kuondoka hapo dukani.

**Swali:** Baada kuondoka nini kilifuata?

**Jibu:** Nilipofika mlangoni wakati naondoka nikakumbuka kwamba niliacha simu yangu na hela, niliporudi kuwaomba wanipatie Sabaya aliagiza wanitoe 'lock' na walinipiga vibao na ilinibidi kuondoka na kuwaachia simu na fedha zangu.

**Swali:** Huyu mtu uliyemwomba akurudishie simu na fedha zako yupoje?

**Jibu:** Huyo mtu alikuwa mweusi, amevaa miwani na kaunda suti ya rangi ya bluu.

**Swali:** Ukimwona leo utamkumbuka?

**Jibu:** Ndiyo.

**Swali:** Hebu angalia watu walipo mahakamani halafu nenda ukamguse mabega.

**Jibu:** Ni huyu hapa aliyesimama karibu na askari magereza.

**Swali:** Je, hizo hela na simu zilizochukuliwa ziko wapi?

**Jibu:** Fedha na simu wanazo wao kwa kuwa waliondoka nazo.

**Swali:** Tukio la nyie kuwekwa chini ya ulinzi lilitokea lini?

**Jibu:** Nakumbuka lilitokea Februari 9 na nilikwenda kuandika maelezo Kituo Kikuu cha Polisi cha Arusha Februari 16, mwaka huu.

**Swali:** Kwa nini ulichelewa kwenda kuandika maelezo kituo cha polisi?

**Jibu:** Kwa kuwa aliyekuja dukani ni Mkuu wa Wilaya ya Hai. Nilipata hofu ya kwenda kituo cha polisi kuandika maelezo.

**Swali:** Ni kitu gani kinafanya umtambue huyo mtu aliyekuja dukani kwamba ni yeye.

**Jibu:** Nitamtambua kwa kuwa ndiye aliagiza nipigwe na alikuwa na huyo mwenzake aliyekaa pembeni yake. Pia yeye ndiye aliyeniambia niondoke na nilipoondoka nilimwona kwa karibu.

Jambo lingine linalofanya nimkumbuka ni pale niliporudi ndani kuomba wanipatie vitu vyangu. Aliagiza nipigwe tena, hivyo nilimtambua vizuri kwa siku hiyo.

**Swali:** Ni nani huyo aliyekuwa anaagiza kwamba utolewe 'lock'?

**Jibu:** Ni Mheshimiwa Lengai Ole Sabaya.

Baada ya hapo, Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, ulimhoji shahidi huyo kama ifuatavyo;-

**Swali:** Unaweza kueleza mahakama umeanza kufanya biashara kwa muda gani?

**Jibu:** Biashara hii nimeanza muda kidogo lakini sikumbuki ni lini.

**Swali:** Nitakuwa sahihi kusema kwamba unafanya biashara bila kuwa na kitambulisho cha machinga?

**Jibu:** Nina kitambulisho cha mwaka jana kwa kuwa cha mwaka huu bado hatujavitapa.

**Swali:** Je, huyo mteja aliyekuja kununua Chandarua Februari 9 mwaka huu alikuja saa ngapi?

**Jibu:** Alikuja majira ya 10.00 jioni.

**Swali:** Unasema ulikwenda dukani kwa Mohamed majira ya saa ngapi na ulikuta watu wangapi?

**Jibu:** Nilikwenda majira ya saa 11:00 jioni lakini idadi ya watu waliokuwapo dukani siifahamu.

# Waziri: Hali inazidi kuwa mbaya corona

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesema kuanzia leo itatangaza rasmi aina za chanjo za corona zitakazotumika nchini kati ya chanjo nane zilizothibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Imesema lengo lake ni kuchanja Watanzania milioni 35, sawa na asilimia 60 kwa kutanguliza makundi ya kipaumbele kama watoa huduma za afya, wazee na watu waliopo katika hatari ya kupata maambukizi.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajina, aliyasema hayo mbele ya waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam alipozungumzia hali ya udhibiti wa UVIKO-19 nchini.

Alisema kuazia leo watawasilisha taarifa ya wapi chanjo hizo zitapatikana na zitatolewa kwa utaratibu na makundi yapi yataanza kupewa katika awamu ya kwanza.

"Lengo letu ni kuwafikia watu angalau milioni 35 sawa na asilimia 60 ya Watanzania wote wawe wamepata chanjo, hata kama tutazidi ni vizuri lakini lengo kufikia hapo," alisema.

Alisema kipaumbele kitakuwa kwa Watanzania ambao wapo mstari wa mbele katika kutoa huduma za mapambano hayo.

"Hata nyie waandishi wa habari mjiandae kesho (leo) mje na madaftari mjifunze na mpate chanjo," alisema.

Waziri huyo alisema suala la uchanjaji litakuwa ni hiari na bure kwa kila Mtanzania atakayehitaji.

Kuhusu hali ya maambukizi ya UVIKO 19 nchini, alisema inaendelea kuwa mbaya kwa sababu watendaji wanaopaswa kutimiza wajibu wao kisheria, hawafanyi hivyo.

Alisema Watanzania hawazingatii afua zilizowekwa na Wizara ya Afya kama kuvaa barakoa, kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

"Serikali haitaendelea kuvumilia viongozi ambao hawatimizi wajibu wao katika kudhibiti maambukizi.

"Tutahimarisha ufuatiliaji na tutafuatilia utekelezaji na wasiyotimiza wajibu wao wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo,"alionya.

Waziri huyo alikiri kuna ulegevu wa hali ya juu katika kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19 kwa kuwa viongozi wa serikali na wananchi hawazingatii taratibu zilizowekwa za kujikinga.

"Mimi ni waziri wenu wa afya, hali siyo nzuri, haya ninayowaambia myazingatie, siwatishi ila ninawaeleza ukweli ili mtimize wajibu wenu kwa kujilinda ili tuendelee na majukumu yetu," alionya.

Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara ya Afya, Dk. Leonard Subi, alisema mapambano dhidi ya ugonjwa huo yakitiliwa mkazo, maambukizi yatapungua ndani ya mwezi mmoja.

Alisema ugonjwa huo unawapata vijana walio chini ya miaka 60 tofauti na virusi vya awamu ya kwanza vilivyokuwa vinawapata wazee peke yake.

Alisema serikali inaendelea na mchakato wa ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha chanjo na siyo kwa ajili ya corona tu. Dk. Subi alisema siyo mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa na kiwanda cha kuzalisha chanjo, akikitaja kilichoko wilayani Kibaha mkoani Pwani, kinachozalisha chanjo sita za mifugo.

Akizungumzia mjadala wa mwongozo wa chanjo, Dk. Subi alisema huo ni utaratibu wa kawaida kwa watoa huduma za chanjo na kinga kutia sahihi kwa hiari kuhusu chanjo hiyo.

"Ni utaratibu wa kawaida kwa utoaji wa chanjo na kinga, hata wanaume wakienda kufanyiwa tohara, ni lazima kutia saini ndipo wafanyiwe tohara," alifafanua Dk. Subi.

Juzi Dorothy alitoa takwimu zinazoonyesha idadi ya wagonjwa wa UVIKO-19 imefika 682 kutoka wagonjwa wa awali 408. Kati yao, 284 wanapumua kwa msaada wa mashine kufikia Julai 21 mwaka huu.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akimsikiliza Balozi wa Palestina nchini, Hamdi Mansour, alipokutana na Mabalozi wanaotoka katika nchi za Kiislamu kwa ajili ya kuhitimisha sherehe za Eid El Haj jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Zitto, Mbatia waomba kuteta na serikali

**Na Enock Charles**

VYAMA vya NCCR-Mageuzi na ACT-Wazalendo vimesikitishwa na kitendo cha kukamatwa na kuendelea kushikiliwa kwa siku mbili kwa viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), huku kikiomba kukaa kwenye meza ya mazungumzo na serikali.

Viongozi wa CHADEMA wanaoshikiliwa hadi sasa ni Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, ambaye Jeshi la Polisi linadai anakabiliwa na tuhuma za kuratibu kundi la kigaidi na njama za mauaji ya viongozi.

Katika tamko lao la pamoja jana, Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia na Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, walisisitiza kuachiwa kwa viongozi hao.

Walidai wanaamini kushikiliwa kwa viongozi hao wa CHADEMA kumetokana na kongamano walililoliandaa kudai Katiba Mpya, wakijikita kwenye misingi ya katiba ya nchi na si vinginevyo.

Kufuatia kukamatwa kwa viongozi hao, vyama hivyo vimetoa wito kwa Jeshi la Polisi kuwaachia mara moja bila masharti huku wakitoa rai kwa wananchi kukemea hali hiyo ambayo inafifisha zaidi utengamano wa kitaifa.

"Tunatoa wito kwa Jeshi la Polisi kuwaachia mara moja bila masharti viongozi wote wa CHADEMA," viongozi wa vyama hivyo viwili walisisitiza katika tamko lao.

Viongozi hao pia walitoa wito kwa viongozi wa serikali na vyama vya siasa kukaa chini na kuzungumza namna ya kufanya siasa bila ya uhasama, walisisitiza: "Ni wakati sasa kwa viongozi kuzungumza (political dialogue)".

# ...Waziri awatoa hofu mabalozi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewaeleza mabalozi njia mbalimbali inazozitumia kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona ikiwa ni pamoja na kuridhia uingizwaji wa chanjo kwa balozi, taasisi na mashirika ya kimataifa yanayotaka kufanya hivyo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alibainisha hayo mbele ya baadhi ya mabalozi wanaotoka nchi za Kiislamu wakati alipokutana nao kwa ajili ya kuhitimisha sherehe za Eid El Haj jana jijini Dar es Salaam.

Balozi Mulamula pia alifafanua kuhusiana na maswali aliyokuwa akiulizwa na baadhi ya mbalozi juu ya chanjo ya kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19, akisema kuwa hakuna balozi, taasisi au shirika la kimataifa lililozuiliwa kuingiza chanjo kwa ajili ya kuwachanja watu wake na kuwasihi kutoa taarifa kwa Wizara ya Afya ili kuwezesha namna bora ya kuratibu na kupokea chanjo hizo.

"Ninaomba niwahakikishie waheshimiwa mabalozi kuwa serikali yetu ni sikivu sana, nimekuwa nikiulizwa maswali mbalimbali kuhusu uingizwaji wa chanjo kwa ajili ya kuwachanja watumishi katika balozi zenu hapa nchini ila ninaomba msisite kuwasiliana na Wizara ya Afya kwa ajili ya kuratibu njia bora ya kupata chanjo hiyo," alisema Balozi Mulamula.

Mbali na mkutano huo, waziri huyo jana alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donnell pamoja na Balozi wa Uingereza nchini, David Concar.

Balozi Mulamula alikutana na mabalozi hao kwa nyakati tofauti katika ofisi ndogo za wizara jijini Dar es Salaam ambapo awali alikutana na Balozi Pamela na baadaye Balozi Concar kwa lengo la kujadiliana masuala mbalimbali ya uhusiano wa kidiplomasia baina ya Tanzania na nchi zao.

Pamoja na mambo mengine, viongozi hao walijadili masuala mbalimbali ya kuendeleza na kuimarisha ushirikiano wa uwili (Bilateral Cooperation).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga onyesheni ubora, burudani fainali FA

**MSIMU** wa 2020/21 unatarajiwa kukamilika kesho Jumapili kwa watani wa jadi nchini, Simba na Yanga kukutana katika mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Yanga ndio ilikuwa ya kwanza kutinga fainali hiyo baada ya kuwaondoka Biashara United ya Musoma mkoani Mara kwa kuwafunga bao 1-0 wakati Simba yenyewe iliichapa Azam FC goli la jioni walipokutana kwenye mchezo wa hatua ya nusu fainali Mjini Songea, Ruvuma.

Simba ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo ambayo yanatoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Fainali iliyopita, Simba ilicheza dhidi ya Namungo FC ya mkoani Lindi na iliibuka na ushindi wa mabao 2-1, mtanange huo ukipigwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Sumbawanga, Rukwa.

Hata hivyo, tofauti na msimu uliopita, mwaka huu timu zote zitashuka uwanjani tayari zikiwa na tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya CAF baada ya Tanzania kupata nafasi ya kuwakilishwa na klabu nne, mafanikio ya Simba yakichangia ongezeko hilo.

Kwanza kabisa tungependa kulipongeza Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa uamuzi wake wa kusambaza mchezo huo katika mikoa mbalimbali hapa nchini, ikumbukwe mwaka 2016, fainali hizo zilichezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri kati ya Simba dhidi ya Mbao, wakati huo ikifundishwa na Mrundi Etienne Ndayiragije.

Kwa kupeleka fainali hiyo Kigoma, TFF na wenyeji Chama cha Soka mkoani huko (KRFA), kimepata nafasi ya kuufanyia matengenezo Uwanja wa Lake Tanganyika ili kufikia viwango vinavyohitajika au kukaribia hadhi ya mchezo huo.

Tunapenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha wamiliki wa viwanja kwa kushirikiana na vyama vya mikoa kuendelea kuvitunza viwanja hivyo hata baada ya kumalizika kwa michezo hiyo ili kuendeleza hamasa kwa wachezaji chipukizi.

Lakini tunafahamu kuwapo kwa mchezo huo, shughuli mbalimbali za kiuchumi zimeimarika kuanzia mapema wiki hii kwa sababu ya mashabiki huhitaji huduma ya malazi, chakula na usafiri wa ndani siku wageni hao watakapoondoka na kurejea walikotoka. Tunazipongeza timu zote mbili kwa kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kusaka ushindi na kuendeleza furaha kwa mashabiki wao, ikiwa ni baada ya siku chache kufungwa kwa pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ili mazuri yote yaliyofanywa yaonekane, ni muhimu kwa wachezaji wa timu zote mbili kuonyesha nidhamu ndani ya uwanja na kucheza soka la burudani.


Mbali na kusaka ushindi, wachezaji wanatakiwa kuutumia vizuri mchezo huo kwa kunadi vipaji vyao na watakaofanikiwa watajiweka katika nafasi nzuri za kuboresha mikataba yao huku wale ambao wako huru, wakawavutia mabosi zao kuwapa mikataba mpya.

Mchezo wa soka kamwe hauhitaji miujiza, timu itakayoonyesha kiwango kizuri, itakayokuwa makini na itakayotumia vyema nafasi itakazozitengeneza, itajiweka kwenye mazingira mazuri ya kushinda taji hilo.

Lakini pia tunapenda kuwakumbusha mashabiki kuwa watulivu na kushangilia wachezaji wao kwa nidhamu. Si busara baada ya mchezo kumalizika, wakaonekana mashabiki wanaotoa lugha za matusi au lawama kwa wachezaji/ viongozi baada ya kupoteza mchezo.

Ni wazi mechi ya kesho inahitaji kupata mshindi, hivyo utulivu na busara vinahitajika wakati wote kabla na baada ya filimbi ya mwisho kupulizwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Bendera ipepeayo sana...

Na barnabas Maro

**WAHENGA** ni wazee wa zamani wenye busara na hekima/hikima. Ni wajuzi wa mambo ya kale waliotegemewa kutoa ushauri katika masuala ya jamii.

"Bendera ipepeayo mwisho huchanika." Methali hii huweza kutumika kumpigia mfano mtu anayejisifu na kujitangaza kwa uwezo alio nao. Hatimaye uwezo huo utaisha na abakie katika hali duni au mbaya.

Ifahamike kuwa 'shabiki' ni mtu mwenye mapenzi na hamasa kubwa juu ya jambo au kitu fulani. Mtu wa namna hii hana mapenzi ya dhati na ya kudumu kwenye timu anayoishabikia ila ni kutaka ushindi tu; kinyume chake anaachana nayo na kuishangilia timu yenye mafanikio katika ushindi. Mtu wa namna hii ni kisebusebu yaani mwenye tabia ya kukataa kitu au jambo ilhali analitaka.

Watu wa tabia hii hawataki kujua jinsi klabu inavyoendeshwa na wachezaji wanavyotunzwa! Ni hodari mno kulalamika, kulaumu, kutukana, tena matusi ya nguoni timu nyingine zinazokuwa na maendeleo.

Nazungumzia timu mbili za Bandari ya Salama (Dar es- Salaam) ziitwazo "watani wa jadi." Maana halisi ya "watani" ni watu wanaofanyiana dhihaka. Watu aghalabu wa kabila tofauti au rafiki mkubwa ambaye ameruhusiwa kumdhihaki mwingine kwa mujibu wa mila zao pasi na aliyetaniwa kukasirika.

Yanga na Simba zilikuwa moja mwaka 1935 kisha zikagawanyika - sio kwa makubaliano, bali kwa kutoelewana. Tangu wakati ule zikawa maadui mpaka sasa unaposoma gazeti hili!

Kuchekana na kuzomeana timu mojawapo inapofungwa na timu za nyumbani (Tanzania) zina haki ya kuchekana na kushangilia mojawapo inaposhindwa na timu za nyumbani

Hata hivyo, kuchekana na kuzishangilia timu za nje ya Tanzania zinapoifunga timu yoyote katika hizo mbili si 'utani wa jadi' bali ni ujinga (hali ya mtu kutojua jambo fulani) na upumbavu yaani utendaji wa mambo yanayokera.

Hali ya kuwacheka ndugu zetu kindakindaki wanaposhindwa na timu za nje ya Tanzania ni ubahaluli yaani upumbavu. Kama nduguyo anapigwa na adui kutoja nnje ya Tanzania kisha unacheka na kumshangilia mgeni huenda una walakini (kasoro iliyo kwenye kitu au mtu; upungufu, ila, dosari) kichwani mwako. Katika yote hayo, hakuna hata moja linaloendana na udugu wa Watanzania! Ukiitwa 'bwege' (mtu mpumbavu, mpuuzi) hutokuwa na sababu ya kulalamika!

'Utani'ni maneno au vitendo vya dhihaka; mzaha. Tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana ukweli na kuimarisha uhusiano wao. Taratibu au desturi za kimila ambazo zinawafanya watu wanaojuana waweze kuambiana au kutendeana jambo lolote la mzaha bila ya kuleta chuki au kero.

Kwa jinsi Simba na Yanga zilivyo sasa, ni vigumu kuamini kuwa eti ni watani wa jadi ilhali 'jadi' ni asili ya mtu; mwenendo wa mtu. Mambo ya asili ambayo watu wa kabila fulani kurithi kutoka kwa mababu zao; asili ya mtu kama vile uzawa, ukoo au nasaba.

Kwa hakika timu hizo hazistahiki kuitwa 'watani wa jadi.' Niwakumbushe wasomaji kuwa maana halisi ya 'stahiki' ni kitendo cha mtu kuwa na haki ya kupata kitu fulani kutokana na ufanisi aliopata.

Neno hilo ni tofauti na 'Stahili; lenye maana ya kitendo cha mtu kupata adhabu kulingana na jambo baya alilofanya.

Yanga na Simba wamekuwa mahasimu kwani ni watu wanaochukiana tangu walipohitilafiana na kutengana kwa takribani miaka 86 iliyopita. Leo wataitwaje 'watani wa jadi'?

Nieleweke kuwa sikatai timu za Simba na Yanga zisizomewe zinaposhindwa na timu za Tanzania, la hasha (sivyo kabisa!) ninachopinga mashabiki wa timu hizo kuchekana na kuzodoana mojawapo inapofungwa na timu za ughaibuni yaani nchi zilizoko mbali na Tanzania. Kwanini twajicheka wenyewe kama majuha?

Ajabu ni kwamba Simba na Yanga zinapokwenda kucheza na timu za mikoani wakazi wa mikoa hiyo huzishangilia mno kuliko timu za mikoa yao.

Takribani mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani kuna matawi ya Simba na Yanga badala ya kuungana na timu za mikoa yao!

Ndo maana wahenga walisema "kipenda roo hula nyama mbichi." Maana yake roho ikipenda huweza kula hata nyama mbichi.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784334096**

## Wanaoharibu majengo makumbusho waonywa

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

SERIKALI amewaonywa wananchi wanaokaa katika majengo mbalimbali ya makumbusho kuacha kuharibu uhalisia wa miundombinu hiyo kwa dhamira ya kubadilisha mwonekano wa asili.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alitoa onyo hilo jana katika eneo la Makumbusho ya Malikale ya Mikindani, mkoani hapa akiwa kwenye ziara ya kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii na kuangalia namna ya kuboresha pasipo kuharibu uhalisia wake.

Alisema kubadilisha uhalisia wa majengo hayo yanayotambulika kama malikale ni sawa na kudhulumu haki ya vizazi vijavyo kutojua wapi nchi yao imetoka na inakokwenda kwa kuwa hakutakuwa na ushahidi wowote wa kuonyesha uhalisia wa nyuma.

Masanja alisema lengo la wizara ni kuona eneo la Mikindani linatambulika kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kuwavutia watalii wengi na kuwashukuru wakazi wa Mikindani kuendelea kutunza majengo ya kale pasipo kuharibu uhalisia wake.

"Kuna maeneo tumegundua wakazi wa kwenye majengo ya makumbusho wanayaharibu makusudi ili wapate nafasi ya kujenga majengo ya kisasa pasipo kupata utaratibu wa namna ya kutunza kumbukumbu iliyopo. Hilo hatutaliruhusu, alisema.

Alisema ni ngumu kuwavutia watalii ikiwa maeneo ya kale yatapoteza uhalisia wake na kuagiza Idara ya Makumbusho ya Taifa kuanza kuweka vyakula vya asili katika maeneo hayo kwa ajili ya kutoa fursa kwa wageni kujifunza utamaduni wa wenyeji yakiwamo mapishi.

Pia alitumia ziara hiyo kumjulia hali Mzee Hassan Kidume, anayetajwa kuwa mwenyeji wa Mwalimu Julius Nyerere katika maeneo hayo ya Mikindani mwaka 1954 alipokuwa katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika.

Awali, Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa, Noel Luoga, alsiema idara imeshaandaa mwongozo wa namna ya kukarabati majengo yote ya makumbusho na kwa sasa wanatarajia kuifikisha kwa wadau Agosti 5, mwaka huu.

# Waziri akerwa na mrundikano wa bodaboda vituo vya polisi

**Na Abubakari Akida**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, ameshangazwa na wingi wa bodaboda katika vituo vya polisi nchini huku akiwataka wananchi ambao mashauri yao yanasikilizika, wafike ili kuondoa msongamano wa vyombo hivyo.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar baada ya kupata maelezo na kutembelea karakana ya kuhifadhia vidhibiti hivyo katika Kituo cha Polisi Madema na kushangazwa na wingi wa bodaboda kituoni hapo.

"Nchi yetu inataka kupiga hatua za kmaendeleo na uchumi. Kwa namna hii ya mrundikano wa bodaboda katika vituo vya polisi maana yake shughuli nyingi za vijana zimesimama. Naelewa kuna vidhibiti kwa ajili ya kesi maalumu ambazo zingine ziko mahakamani, hivyo haviwezi kuachiwa lakini kwa vile ambavyo kanuni na sheria inaweza kuviruhusu basi viondoke.

"Natoa wito kwa wananchi kufika vituo vyote vya polisi nchi nzima na kufanya mazungumzo na wakuu wa vituo ili tuondoe mrundikano huu. Kila mkoa ninaotembelea nakuta vituoni kuna mrundikano wa bodaboda," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Unguja, Awadh Juma Haji, alisema vyombo vingi vilivyoko kituoni ni kutokana na waliovitendea makosa kutofika kwa wahusika wakuu hali inayosababisha kuwapo hapo na kukiri kuwa ni kero kwa jeshi.

"Mheshimiwa Naibu Waziri hapa vyombo vilivyopo ambavyo tunavishikilia hatuwezi kuvitoa ni vile ambavyo mashauri yake bado yako mahakamani. Lakini kuna vingine watuhumiwa wake wamekimbia tangu vikamatwe. Tunachofanya tunasubiri ule muda wa kisheria wa miezi sita ili taratibu za utaifishaji zifanyike.

Hapa tuna magari ya wizi, bodaboda zingine zimeshiriki katika makosa ya usalama barabarani zingine zimehusika kwenye uporaji na tatizo lingine wahusika hawaji vituoni kuonana na wakuu wa vituo kuchukua vyombo vyao hali hiyo husababisha mrundikano huu," alisema.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadh Juma Haji (kushoto) akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamis Hamza Chilo, alipotembelea Kituo cha Polisi Madema Zanzibar jana, ambapo ameagiza wananchi kufika vituoni kuchukua vyombo vyao kwa mujibu wa taratibu na sheria ili kupunguza mrundikano wa vyombo hivyo vituoni. **PICHA: WMNN**

# Ataka maofisa kujibu hoja za ardhi

**Na Munir Shemweta,** MTWARA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka watendaji wa sekta ya ardhi kushiriki katika ziara za viongozi ili kujibu changamoto zitakazojitokeza wakati wa ziara.

Akizungumza na watendaji wa mkoani Mtwara jana, Dk. Mabula aliwataka kuhakikisha wanakuwa na daftari maalum la kuorodhesha migogoro ya ardhi na hatua zilizochukuliwa sambamba na kuandika taarifa kuhusiana na migogoro kwenda ofisi za wakuu wa wilaya.

"Kiongozi akija eneo lako hakikisha uko katika msafara. Suala la ardhi likijitokeza basi utoe ufafanuzi ili hatua zichukuliwe," alisema.

"Kumekuwa na utaratibu akija kiongozi mpya migogoro inaibuka upya. Sasa mhakikishe migogoro hiyo inaandikwa kwenye mfumo wa 'matrix' ili kumrahisishia kiongozi na kumwepusha kupokea malalamiko yaliyokwishafanyiwa kazi," aliongeza.

Katika kuhamasisha wananchi kulipa kodi ya ardhi, Dk. Mabula alizitaka halmashauri kuandika taarifa ya jinsi zilivyotoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kama vile redio za kijamii.

Pia aliwaeleza watendaji wa sekta ya ardhi katika mkoa wa Mtwara kuwa anafikiria namna ya kuanzisha ushindani wa ukusanyaji kodi ya ardhi katika halmashauri kwa lengo la kuona halmashauri iliyofanya vizuri zaidi.

Katika kujenga nidhamu ya watumishi, Dk. Mabula aliagiza watumishi wa sekta ya ardhi kutotoka nje ya vituo vya kazi bila wakurugenzi kuwa na taarifa na kusisitiza kuwa watumishi wa ardhi wanatakiwa kutatua migogoro na si kuwa sehemu ya migogoro.

Akielezea upangaji miji katika maeneo mbalimbali nchini, alisema pamoja na wizara kusaidia harakati za upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi katika halmashauri, jukumu la upangaji linabaki kwa halmashauri kwa kuwa ndiyo mamlaka husika.

"Si jukumu la wizara kuingilia upangaji wa miji katika halmashauri ila inazisaidia kuzikopesha fedha na kueleza kuwa ziko halmashauri zilizopewa Sh. milioni 200 hadi 300 lakini zipo zingine zimetumia fedha kwa mambo mengine. Nasisitiza pesa ziende katika masuala ya ardhi," alisema.

Mmoja wa wananchi wa Mtwara, Sheikh Nurdin Manguji, anayemiliki takriban hekta 8.704 katika eneo la Shangani West, aliomba serikali kupitia Wizara ya Ardhi kumsamehe kodi anayodaiwa miaka ya nyuma kwa kuwa hakuwahi kufahamishwa na kupatiwa nyaraka za eneo lake.

## Washauri wakulima kupunguziwa gharama

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WANAFUNZI wa Kitanzania wanaosoma Chuo Kikuu cha Kilimo cha China (CAU), wameiomba serikali kuangalia namna ya kuwapunguzia gharama ya uzalishaji wakulima ili kuendana na kipato chao.

Chuo hicho kinatekeleza mradi wa pamoja wa kupunguza umaskini kwa wakulima wadogo mkoani morogoro.

Wanafunzi hao wanaosoma kwa njia ya mtandao kutokana na changamoto ya usafiri iliyosabishwa na ugonjwa wa corona, walitoa rai hiyo juzi baada ya kufanya ziara ya mafunzo kwa vitendo katika vijiji mbalimbali vinavyotekeleza mradi huo mkoani hapa.

Ziara hiyo ililenga kuangalia namna chuo hicho kinavyotekeleza miradi mbalimbali hasa ya kilimo cha mahindi katika kusaidi kuwapunguzia wakulima umaskini kwa utoaji mafunzo ya uzalishaji wa mazao kwa tija. Mmoja wa wanafunzi hao, Juliet Frank, alisema licha ya mradi huo kuwanufaisha wakulima wengi baada ya kupata elimu ya kilimo cha kisasa, kuna haja ya wataalam kuangalia namna bora ya kuwapunguzia gharama za uzalishaji.

Mwanafunzi huyo aliomba serikali ya mkoa kwa kushirikiana na chuo hicho kinachotekeleza mradi wa pamoja endapo gharama zitapungua zaidi katika uzalishaji zitasaidia kupunguza umaskini kwa wakulima wadogo hasa kupitia kilimo cha mahindi.

"Licha ya mradi huu kuwasaidia wakulima wadogo, kuna kila sababu ya kutafuta njia mbadala ya kuwasaidia wakulima kupunguza mzigo wa kazi, kuwapo na vitendea kazi kama mashine za kupandia na kupalilia mahindi kama ilivyo katika mazao mengine. Hii itasaidia kuokoa muda," alisema.

Naye Mwanafunzi Salma Shehe, alisema mabadiliko ya tabia nchi yamekuwa wakiwaathiri wakulima wadogo pale mvua zinapokosekana au kuzidi kiwango na kusababisha mazao kuharibika yakiwa shambani, hivyo kuwasabishia hasara.

Awali, Mratibu wa mradi huo, Ernest Mkongo, alisema utekelezaji wa mradi huo ulianza mwaka 2011 kwa kuanza na kijiji cha Peapea wilayani Kilosa na baadaye kuhamishiwa katika kijiji cha Mtego wa Simba wilayani Morogoro mwaka 2014.

Mkongo alisema kupitia mradi huo, wakulima walijifunza njia za kisasa na kuwawezesha kuvuna magunia 18 ya mahindi kwa ekari moja kulinganisha na awali wakivuna magunia manne hadi matano kwa ekari moja.

"Teknolojia walizofundishwa zimesaidia kuongeza tija kwa kiasi kikubwa mara tatu zaidi ya awali. Mkulima alikuwa anaambulia magunia matano pekee kwa ekari moja na kubwa zaidi elimu ile haikuishia kwa wanufaika wachache bali hadi wanakijiji wengine ambao walijifunza kupitia kwa wenzao," alisema Mkongo.

Alisema baada ya mafanikio katika majaribio hayo, mradi ulipanuka na kuvifikia vijiji nane kutoka katika wilaya zote za Mkoa wa Morogoro katika kipindi cha mwaka 2018 hadi mwaka 2021.

Mkongo alivitaja vijiji vingine na wilaya zake kwenye mabano ni Letugunya na Ngayaki (Gairo), Kitete (Kilosa) , Kisegese (Kilombero) , Kiswago (Malinyi), Kikundi (Morogoro), Makuyu (Mvomero) na Mwaya, Wilaya ya Ulanga,

# Waandishi wachanga wafundwa kujiepusha vitendo vya ukatili

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Rose Reuben, amewataka waandishi wa habari wachanga kujiweka mbali na vitendo vya ukatili wa kingono ndani ya vyumba vya habari.

Reuben alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kutoka mikoa Morogoro, Dodoma, Dar es salaam, Mwanza na Singida juu ya ukatili wa kingono ndani ya vyumba vya habari.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na TAMWA kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Kusaidia Vyombo vya habari (IMS) na kufanyika mkoani hapa.

Mkurugenzi huyo alisema kwa mujibu wa mdahalo uliofanyika juzi mkoani hapa wa kuangalia matendo ya ukatili wa kingono kwenye vyumba vya habari, wanahabari walionekana kuwa na nafasi ya 11 kati ya kura 21 zilizopigwa kutoka kwa wanahabari. Kati yao wanaume walikuwa wanne ikitofautishwa na wahariri na wamiliki wa habari waliopata kura 13.

"Mwanahabari mchanga anayetoka chuoni akiingia kwenye chumba cha habari na kukubali kufanyiwa ukatili wa kingono lazima ataendeleza matendo hayo pale atakapopata nafasi ya kuwa mhariri, hali hiyo haitakoma," alisema Reuben.

Alisema wingi wa changamoto hiyo kwa wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari kushika nafasi ya 13 ni chachu ya kuonyesha kuwa changamoto hiyo inaanzia chini kwa wanahabari wenyewe.

Mkurugenzi huyo alisema wanahabari wanapaswa kuendelea kujifunza masuala ya ukatili wa kijinsia ili kuacha kufanyiwa au kufanya matendo ya ukatili wa kingono wakiwa kazini na kwamba wakiendekeza wanaweza kuingiza tabia hizo hata mitaani wanakoishi na kushindwa kuielimisha jamii juu ya vitendo hivyo.

Aliwataka wanahabari kujenga tabia ya kuripoti kwenye vyombo vya sheria matukio ya kingono wanayofanyiwa. Alisema licha ya kutungwa kwa sheria, ukatili wa kingono ni kosa la jinai lakini hakuna hata mwanahabari mmoja aliyejitokeza kutoa taarifa.

Awali, Katibu wa Klabu ya Waandishi Mkoa wa Morogoro (Moro- PC), Lilian Lucas, aliomba serikali kutambua kuwa wakati umefika wa kusaidia na kuondoa suala la ukatili wa kijinsia kwenye vyombo vya habari nchini.

Lucas alisema mdahalo uliofanyika wa wanahabari umewasaidia kujifunza mengi na kwamba watakuwa mstari wa mbele kufichua masuala ya ukatili wa kijinsia yanayowakumba na kuiambia serikali kwa uwazi.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Juma Mtanda, aliishukuru TAMWA kutoa mafunzo hayo ambayo ana imani yatamsaidia kuboresha kazi zake za kila siku.

Alisema elimu ya masuala ya jinsia na vyombo vya habari, uongozi wa mwanamke na maendeleo na misingi ya uhuru wa kuandika habari itawasaidia wanahabari kuimarika katika majukumu yao ya kila siku na kuepuka kuingia kwenye migogoro ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni.



Mkulima wa mbegu za asili wa Karatu, Arusha Elibaraka Joseph (kulia) akiwaonyesha washiriki bidhaa hiyo, kwenye mkutano wa mifumo ya chakula 2021 jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TAKUKURU yaonya wananchi utapeli

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imewataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya matapeli wanaojifanya ni maofisa wa taasisi hiyo. Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, alitoa tahadhari hiyo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utendaji kazi wa miezi mitatu kwa waandishi wa habari.

Raymond alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakipigiwa simu na watu wanaodaiwa maofisa wa TAKUKURU wakitakiwa kufika kwenye ofisi za taasisi hiyo na wanapofika wanakuta hakuna taarifa za wito wao.

"Wananchi kuweni makini na watu wanaojifanya ni maofisa wa TAKUKURU. Mkipata taarifa ya wito pigeni namba yetu kutoa taarifa tushughulikie kupata uhakika mapema kabla watu hao hawajazima simu zao," alisema

Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema watu hao baada ya kupiga simu kwa wananchi, wanazima simu na hawapatikani tena jambo ambalo linasababisha usumbufu

Alisema wanaendelea kufayanyia kazi malalamiko hayo ya wananchi na hadi sasa ni mtuhumiwa mmoja pekee aliyekamatwa na kesi yake inaendelea kusikilizwa mahakamani.

Raymond alisema katika kipindi cha miezi, mitatu Aprili hadi Juni, mwaka huu, wamepokea malalamiko 127 kati ya hayo, 57 uchunguzi wake unaendelea na 70 hayahusiani na taasisi hiyo.

Alisema katika kipindi hicho, kesi 15 ziliendelea kuendeshwa katika mahakama mbalimbali za mkoa wa Pwani na kwa miezi hiyo kesi sita zilitolewa uamuzi na Jamhuri ilishinda na washitakiwa walitakiwa kulipa faini au kutumikia kifungo.



## HABARI DODOMA

## Pinda ataka PASS Trust kujitangaza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, ameitaka Taasisi ya PASS TRUST kutumia wiki yao ya maonyesho kuwatembelea wakulima wa maeneo mbalimbali ili kujitangaza shughuli wanazofanya.

Pinda aliyasema hayo jana wakati akifungua wiki hiyo inayofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square jijini hapa.

Alisema wakulima wengi hivi sasa hawaijui PASS inafanya nini dhidi yao, hivyo ni vyema katika wiki hii kutumia nafasi hiyo kujitangaza ili wajasiriamali wakulima kuwatambua na kutumia fursa ya kupata mikopo.

"Nawaomba mtumie hii wiki kutoa elimu ya utambuzi kwa wakulima,kwa sababu wengi hawawajui,"alisema Pinda.

Alisema wakulima wengi hawajui taasisi hiyo inafanya nini na kwamba wakiwatembelea wakulima pembezoni basi itawasaidia kujitambulisha kwa wajasiriamali ambao ni wakukima na kuwaeleza nini wanafanya na wao watajitokeza kupata fursa za kilimo.

Aliwapongeza kutokana na kujikita katika kusaidia wajasiriamali kwenye shughuli za kilimo.

Alisema jitihada wanazofanya kusaidia serikali kuwekeza katika sekta ya kilimo zinapaswa kuendelezwa na kuungwa mkono ili kuwasaidia wakulima.

Mwenyekiti wa Bodi ya PASS, Dk. Tausi Kida, alisema taasisi hiyo ipo bega kwa bega na sekta ya kilimo ndiyo maana wameanzisha wiki ya PASS ili kutoa elimu kwa wajasiriamali.

Dk. Kida alisema lengo lake ni kuona wakulima wanaufaika na huduma zinazotolewa na taasisi hiyo katika maeneo mbalimbali hapa nchini lengo ikiwa ni kuinua sekta ya kilimo.

Alisema taasisi yao inajishughulisha na wakulima wadogo, wakubwa na wa kati hivyo wanapaswa kuchangamkia fursa ya mikopo ambayo inatolewa na PASS Leasing ili kuinua kilimo chao cha kila siku.

# RC ataja mwarobaini wa mikopo umiza kwa walimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameitaka Benki ya Biashara ya Mwalimu (MCB) kuja na njia itakayowasaidia walimu kupata mikopo yenye masharti nafuu na kwa haraka ili kuondokana na mikopo umiza.

Mtaka aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizindua bidhaa mpya ya Mwalimu na Ujasiriamali iliyoanzishwa na benki hiyo kwa ajili ya kukopesha mashine za uzalishaji mali.

Alisema walimu wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu kutokana na aina ya mikopo wanayokopa kutoka katika taasisi ambazo zina masharti magumu na riba kubwa.

Kwa mujibu wa Mtaka, hali hiyo imewafanya walimu kwa muda mrefu kukabiliwa na madeni kutokea taasisi hizo hali ambayo baadhi yao wanalazimika hata kuhama katika vituo vyao vya kazi.

"Lazima ninyi kama Benki ya Mwalimu mwangalie mnakuja kwa utofauti gani na taasisi zingine za kifedha ili kuwakopesha walimu wenye uhitaji kwa ajili ya mambo mbalimbali yanayowakabili bila kuwapatia usumbufu wowote," alisema Mtaka.

Pia alisema imefikia hatua walimu wanakabidhi kadi zao za benki kwa taasisi za fedha na mishahara inapoingia tu kiasi chote cha fedha kinachukuliwa kwa makato.

Vile vile alisema kuwa benki hiyo inatakiwa kujikita katika kuhakikisha kuwa inakuwa na kitu cha utofauti ambacho kitawavutia walimu na kujiunga nayo.

"Hili jina la mwalimu benki mnaweza kuendelea nalo lakini lazima muone kuwa utendaji wenu uwe kwa ajili ya makundi yote ili kushindana na benki zingine zaidi ya 50 zilizopo nchini," alisema.

Mtaka pia alisema akiwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu alikuwa anapokea kesi nyingi za walimu kukimbia vituo vyao vya kazi kutokana na madeni hali ambayo inaathiri taaluma katika mkoa husika.

"Kuna vituo vya kazi walimu hawafiki kwa kuhofia kuwa wanaowadai watakuja kudai mikopo yao tena unakuta mwalimu kakopa milioni mbili anakatwa milioni saba," alisema.

Akizungumzia mpango huo wa mikopo ya mashine za uzalishaji mali, alisema ni ubunifu mzuri ambao kama utasimamiwa vizuri utawawezesha walimu kustaafu wakiwa na tabasamu.

Kadhalika, aliwataka walimu kuchangamkia mkopo huo wa vifaa ambao utawasaidia kujikwamua kiuchumi.

Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Richard Makungwa, alisema wamejikita katika kutoa huduma za kifedha kwenye ikolojia ya elimu ikiwa pamoja na vyuo vya elimu, walimu, shule, taasisi za elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na TAMISEMI.

"Mwalimu Commercial Bank iliandaa mkakati wa muda mrefu ukiwa na malengo ya kuboresha huduma zenye ubunifu katika kuwafikia wateja wetu," alisema Makungwa.

Alisema moja ya maeneo yaliyopewa kipaumele ni kuwa na bidhaa zinazolenga moja kwa moja mahitaji ya walimu katika kujiinua kiuchumi na kuleta tija kwenye jamii.




Mkazi wa Jiji la Dodoma, akinawa maji tiririka kwenye moja ya masinki katika lango kuu la kuingia kwenye Soko Kuu la Majengo jijini humo jana, ambapo asilimia kubwa ya mabomba yake ni machakavu na hayatoi maji. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Chanzo cha migogoro ardhi chatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amesema asilimia 42 ya migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma inatokana na madai ya fidia kwa wananchi wanaotakiwa kupisha ujenzi wa miundombinu ikiwamo barabara na reli.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa ikiwa ni zaidi ya wiki mbili tangu ahamie Dodoma akitokea Wilaya ya Mpwapwa, Shekimweri alisema amepokea nyaraka za madai ya fidia ya takribani Sh. bilioni 38 na anajiridhisha uhalali wa madai hayo.

Alisema tayari ameshatembelea baadhi ya maeneo ikiwamo Iyumbu na Nytuka na kuzungumza na wananchi kama wakati wa mchakato wa kupima maeneo yao walishirikishwa na wanaridhika na kilichoandikwa.

Shekimweri alisema aliamua kujiridhisha kutokana na jiji kukumbwa na migogoro mingi ya ardhi hasa inayohusu fidia, hivyo kwa kutembelea kwake maeneo hayo na kuzungumza atajua hali halisi na ukweli wa madai ya fidia hiyo.

"Nimeamua kutembelea baadhi ya maeneo na kubaini kwamba yako madai ya fidia ya kweli. Mfano maeneo inapopitishwa reli ya kisasa, reli ya uhuru na barabara ya mzunguko wa nje, lakini yapo madai ambayo wadai walishapokea fidia zamani na hivyo hayo yanatakiwa kuangaliwa upya," alisema.

Aliwaonya wananchi ambao watalipwa fidia, kugawa fidia katika sehemu mbili, ya kwanza wakanunue ardhi katika maeneo ya pembezoni na sehemu ya pili wakawekeze katika kilimo cha zao la mkakati la zabibu.

Shekimweri alisema wananchi wenye madai ya fidia wanatakiwa kuwa watulivu na amani ili ajiridhishe kwanza kabla ya kusaini madai hayo kwani akisaini kabla kuwa na uhakika wa madai atazalisha migogoro mipya badala ya kupunguza.

"Kama kiongozi wa ulinzi na usalama wa wilaya, msimamizi wa ilani ya CCM katika wilaya lazima niwe mbunifu katika kuunga mkono kampeni ya Halmashauri ya Jiji ya kupunguza migogoro hasa hiyo ya fidia," alisema.

Shekimweri alisema pia katika kupunguza kama si kumaliza migogoro ya ardhi jijini hapa, timu maalum kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI inashughulikia baadhi ya migogoro hiyo.



# Zanzibar yazindua chanjo ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, imezindua chanjo ya corona aina ya SINOVAC kutoka China huku idadi ya wagonjwa wa maradhi hayo wakiongezeka hadi kufikia sita.

Akizindua chanjo hiyo jana katika kituo cha upimaji corona, Lumumba Mkoa wa Mjini Magharibi na kuwa kiongozi wa kwanza kuchanjwa, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Mazrui alisema wananchi wanapaswa kuendelea kuchukua tahadhari na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ikiwamo kuvaa barakoa na kujiepusha na mikusanyiko isiyo ya lazima.

Alisema chanjo hiyo haina madhara yoyote kwa binadamu na kwamba Shirika la Afya Duniani (WHO), limethibitisha kuwapo usalama wa chanjo hiyo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Wizara ya Afya Zanzibar imeikubali na kwa sasa zipo dozi 100,000 za chanjo ya Corona.

Pia alisema baada ya wiki mbili, chanjo nyingine itawasili Zanzibar na kwa sasa chanjo itakayotolewa ni kwa awamu ya kwanza.

Katika hatua nyingine, SMZ inatarajiwa kupokea chanjo 100,000 za corona ikiwa ni msaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo ofisini kwake, Vuga jijini Zanzibar wakati akipokea stakabadhi ya msaada huo wa chanjo kutoka kwa Balozi Mdogo wa China anayefanyia kazi zake Zanzibar, Zhang Zhisheng.

Hemed alisema chanjo hizo aina ya SINOVAC zinatarajiwa kuwasili Zanzibar ndani ya muda mfupi baada ya kupokea stakabadhi na ada ya kuwasili, zinatakibidhiwa kwa wizara ya afya ambayo ndiyo yenye dhamana ya musuala ya afya.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itapokea chanjo hizo, ikiwa ni katika juhudi za kujikinga na maradhi ya COVID-19 kwa lengo la kuwakinga wananchi wake kutokana na virusi vinavyosababisha maradhi hayo.

Akizungumzia ubora wa chanjo hiyo, Hemed aliwahakikishia wananchi wa Zanzibar kuwa ni salama na imethibitishwa na WHO kwa ajili ya matumizi.

Naye Balozi Mdogo Zhang alisema China imejipanga kutoa chanjo ili kusaidia kinga dhidi ya COVID-19 na alimhakikishia Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kuwa chanjo hizo ni salama kutokana na kupatikana kwa ruhusa ya matumizi kutoka WHO.

Aidha, alisema China itaendeleza ushirikiano wake na Tanzania ili kuisaidia Zanzibar kukuza uchumi wake na kwamba serikali ya nchi hiyo imejipanga kuisaidia Zanzibar katika kuwekeza kwenye sekta ya viwanda ili kuinua uchumi wa Zanzibar na watu wake.



Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, akipatiwa chanjo ya ugonjwa wa corona aina ya Sinovac kutoka China na Muuguzi Arafa Abdulhakim wa kituo cha kupimia corona kilichopo Lumumba, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Watalii waongezeka licha tishio la corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya dunia kukabiliwa na janga la corona, idadi ya watalii walioingia Zanzibar kwa Juni, mwaka huu, imeongezeka na kufikia 20,416 ikilinganishwa na 9,280 walioingia Machi, mwaka huu.

Akitoa takwimu za uingiaji wa wageni kwa waandishi wa habari ofisini kwake Mzazini, Mkuu wa Takwimu za Kiuchumi kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Abdulrauf Ramadhani Abeid, alisema Ufaransa inaongoza kwa kuleta watalii wengi Zanzibar.

Alisema wageni 11,588 waliongia nchini ni kutoka Ulaya ambao ni sawa na asilimia 56.8.

Alisema kwa mwezi huo, Ufaransa iliongoza kwa kuleta wageni 2,232 sawa na asilimia 10.9 ya wageni wote ikifuatiwa na Poland 2,101 sawa na asilimia 10.3.

Wageni waliongia Zanzibar kwa kutumia usafiri wa boti kupitia Bandari ya Malindi, alisema walikuwa 5,152 sawa na asilimia 25.2 na waliongia kupitia viwanja vya ndege ni 15,264 sawa na asilimia 74.8.

"Asilimia 99.4 ya wageni walikuja kwa ajili ya mapumziko, asilimia 0.5 kwa ajili ya kuwatembelea ndugu na marafiki zao na asilimia 0.1 ya wageni walikuja kwa sababu zingine," alisema Abeid.

Naye Dk. Estella Ngoma Hassan, Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), alisema kuwako kwa idadi kubwa ya wageni kutoka Ufaransa kumetokana na nchi hiyo kuondoa vikwazo vya kusafiri katika nchi yao na kusababisha kuondoka nchini na kwenda nchi zingine. Alisema hali imesababisha Zanzibar kupata wageni wengi kutoka nchini humo.

Aidha, alisema sababu nyingine iliyofanya wageni kutoka Ufaransa kuwa wengi ni pamoja na kuanza chanjo ya corona nchini humo.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Abdulla Mohammed Juma, alisema kamisheni hiyo imebadilisha mikakati ya soko la utalii ambapo awali walikuwa wakitegemea watalii kutoka Ulaya.

Alisema mikakati hiyo imeanza kuzaa matunda na kwamba wageni mbalimbali wamekuwa wakiongezeka.

Pia alisema kuwa kwa miaka sita iliyopita nchi iliyokuwa ikiongoza kuingiza watalii kwa wingi Zanzibar ni Italia lakini kwa sasa idadi imepungua kutokana na corona.

# Waziri ataka matokeo bora ufundi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, ameutaka uongozi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya Mtambwe kufanya kazi kwa bidii itakayosababisha kupatikana mafanikio kwa wanafunzi wa awamu ya kwanza.

Simai aliyasema hayo jana wakati akizungumza na uongozi wa chuo hicho wakati wa ziara aliyoifanya chuoni hapo na kujionea shughuli mbalimbali zikiwamo za masomo.

Akizungumza na wafanyakazi, Simai aliwataka watendaji hao kukabiliana na uhaba wa wafanyakazi kwa kufanya kazi kwa bidii ili mafanikio yapatikane kupitia wanafunzi wa awali.

Alisema moja ya fani zinazotolewa katika chuo hicho ni uvuvi ambayo inalenga kuwaandaa vijana kufikia malengo ya serikali kuelekea uchumi wa buluu.

Simai alielezea matumaini yake kuwa bwawa linalotarajiwa kujengwa kwa ajili ya mafunzo ya vitendo, litatoa fursa kwa wanajamii kujifunza kuogelea ili kuongeza nafasi zaidi katika fani hiyo.

Pia aliutaka uongozi, wafanyakazi na wanafunzi wa chuo hicho kutunza mazingira kwa kupanda bustani na miti mbalimbali ili kuboresha mandhari ya chuo.

Ofisa Mdhamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Moh'd Nassor Salim, aliwataka wanafunzi kuitumia vyema fursa waliyoipata kwa kuweka historia si tu ya kuwa wanafunzi wa mwanzo bali kufaulu vizuri masomo yao.

Naye Kaimu Mratibu Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, Othman Zaid Othman, alisema chuo kimeshafanya usajili kwa wanafunzi 175 wa awamu ya mwanzo ambao wameshaanza masomo katika fani mbalimbali.

Alizitaja baadhi ya fani hizo kuwa ni kilimo, umeme, ufundi magari, useremala na mapokezi huku fani ya uvuvi ikiwa na wanafunzi 50.



ALI KIBA

Uk.14



# GOTI LA MSAMAHA

# Harmonize, Salah njia nyeupe



BAADA ya kupitia vikwazo vingi kwenye mapenzi, hatimaye mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize, ameamua kupiga magoti kuomba msamaha kwa aliyekuwa mkewe Salah Michelotti.

Harmonize na salah walidumu katika mapenzi kwa muda wa miaka minne, lakini ndoa yao ilivunjika baada ya msanii huyo kutangaza kuwa na mtoto na mwanamke mwingine.

Katika kujifariji, Harmonize aliingia katika uhusiano na mwigizaji Kajala Masanja, kabla ya kumwagana katika hali ya kutia aibu.

Kupitia akauti yake ya Instagram, mwimbaji huyo anayetamba kwa sasa ameweka sehemu ya wimbo wake mpya ambao una ujumbe mzito wa msamaha kwa Salah."Samahani ni neno pekee ninaloweza kusema kwako mwanamke mrembo alienipatia miaka minne ya maisha yake nami nikampatia minne yangu, tulipitia mengi ila itoshe kusema nilizingua sanaa ...!"

Anaendelea kusema katika wimbo huo, "Mpaka mungu alipoamua kuniletea mtoto wangu wa kwanza Zuuh na ndio ikawa mwisho wa safari yetu ya pamoja, ndio kuteleza kunatokea na muungwana huomba radhi, ila ningeonekana mjinga zaidi ningeendelea kumficha mtoto wangu,"

Wimbo huo ambao utakuwa ndani ya Albam yake mpya, inaonyesha jinsi mwanamuziki huyo alivyoamua kuficha ya kale na kuomba nafasi nyingine kwa Salah.

Hata hivyo, Salah ameonekana yuko kimya akishughulika na biashara zake licha ya baadhi ya mashabiki wake kumuomba kutoa kauli kuhusu msamaha huo.

BASI SAWA

## Waluguru wanatamani kujitanua Dar



BENDI ya Waluguru Original ya mjini Morogoro, inasaka sehemu ya kukutana na mashabiki wake kila Jumapili jijini Dar es Salaam, kama njia ya kujitanua kisanaa.
Mkurugenzi wa bendi hiyo, Killer Man, amesema wakati umefika wa kujipima na bendi za jijini humo kutokana na uwezo wao kuwa mkubwa.
"Dar es Salaam ni jiji la starehe, hivyo tunaendelea na mikakati ya kusaka ukumbi wa kufanya bonanza kila Jumapili ili kujitambulisha zaidi kwa mashabiki wa dansi," amesema Killer Man.
Amesema, uzoefu waliupata hivi karibuni katika onyesho la Wafia Dansi, lililohusisha baadhi ya bendi za Dar es Salaam, unawatosha kujitanua zaidi.

## Sasa zamu ya Stamina



WIMBI la wasanii wa Bongo Fleva, kuachia Albam zao mpya linazidi kushika kasi, sasa ni zamu ya rapa Stamina Shorwebwenzi, kuachia kazi yake.
Kupitia akaunti yake ya Instagram, Stamina amewataka mashabiki wake kuwa tayari kwani kazi ya kuandaa Albam hiyo imekamilika kwa asilimia mia.
"Kuna haja ya kuongea sana napokutana na wamemchokoza, tumemaliza kazi yetu bado kazi yenu ya masikio sasa, Album imekamilika" ameandika.
Baadhi ya wanamuziki walioachia Albam zao ni Dogo Janja, Weusi, Abbah,Marco Chali, Alikiba, Diamond, Harmonize, Country Wizzy, Stamina, Ibraah, Killy Moni Centrozone.



# Ali Kiba usiwape 'Jealous' wabaya

ILE badika bandua ya Ali Kiba, inazidi kuchanja mbuga na sasa mashabiki wake wanafurahia singo yake mpya inayoitwa jealous.
Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Alikiba amewashukuru mashabiki wake kwa kuupokea vizuri wimbo huo na kuwaahidi atakuwa sawa na mwendo kasi.
Ngoma ya mwisho ya Alikiba inaitwa salute aliyoichia June 30 ambayo alimshirikisha Rude Boy kutoka Nigeria.



# Vanessa utawaweza walimwengu?

KUPATA mtoto ni suala la furaha kwa kila mtu, lakini kwa mwanamuziki Vanessa Mdee, imekuwa sawa na usumbufu kiasi ambacho imembidi kupaza sauti.
Hivi karibuni umeibuka taarifa kwamba mrembo huyo ambaye kwa sasa anaishi Marekani, amejifunguа mtoto na mpenzi wake Rotimi.
"Sina mtoto mnamsumbua tu mama wa watu, yupo zake Arusha mnaanza kumpanikisha kwamba nimezaa, aliyewaambia nimezaa ni nani" amesema Vanessa baada ya mama yake kuja juu kutokana na taarifa hiyo.
Huu ni mwaka wa pili na Vanessa Mdee na Rotimi tangu waanze mahusiano yao na tayari wameshachumbiana lakini mashabiki wao wamekuwa wakitamani couple hiyo ipate mtoto.

# Wabongo walilia madebe

**Na Adam Fungamwango**

HAIKUWA wiki nzuri kwa mashabiki wa muziki wa zamani aina ya 'mafunk' Afrika nzima, baada ya mwanamuziki mkongwe aliyetesa kwa muziki huo miaka ya 1980 hadi katikati ya miaka ya 1990, Pat Shange, kufariki dunia kwa ugonjwa wa COVID-19, unaosababisha kwa na virusi vya corona.
Kwa mujibu wa mkewe Patricia Shange, mwanamuziki huyo alifariki siku ya Jumanne, Julai 15 kwenye Hospitali ya Chris Hani Baragwanath nchini Afrika Kusini.
Mwanamuziki huyo alifariki dunia akiwa na miaka 65.
Pat Shange alivuma miaka ya 1980 na 1990 kutokana na kutoa ngoma zake kali zilizotetemesha bara zima la Afrika.
Picha zake ambazo zilikuwa maarufu kwenye kanda za kaseti akiwa amepiga 'pamba' huku akiwa amenyoa 'panki' na kuweka dawa ya kulainisha nywele zilizidi kumfanya kuwa maarufu kutokana na mwonekano wa kipekee.
Nchini Tanzania ngoma za Pat Shange zilitesa vilivyo kwenye kumbi mbalimbali za disco nchini Tanzania.
Mfano Dar es Salaam kulikuwa na kumbi la kuruka majoka au kuruka 'ndebe' kama walivyokuwa wakisema wakati huo watoto wa mjini kwenye kucheza ngoma zake na wapinzani wake Wasauzi wenzake wakati huo kama vile Sello Chicco Twala, Yvonne Chaka Chaka, Sipho Mabuse na Steve Kekana.
Wakati huo tayari Souzi kulikuwa na wanamuziki kama Pamela Nkuta na wengineo wengi.
Kumbi hizo ni Maggot, YMCA, Msasani Beach Club, Rungwe Ocean ya mzee Mwakitwange, na nyingine nyingi.
Huu ndiyo wakati ambao Bongo ilikuwa inachemka kama bahari. Ndiyo maana kifo cha Pat Shange kimegusa vijana wengi wa zamani, hasa waliokuwa vijana au watoto kwenye miaka hiyo ya mwishoni mwa 1980 hadi katikati ya 1990.
Hizi ni baadhi ya ngoma zake ambazo Wabongo wengi walizipenda.

**I'M NOT CASSANOVA**
Huu ni moja wimbo wake bora ambao ulipendwa sana kwenye klabu nyingi za disco zamani.
Disco haliwezi kumalizika bila ya wimbo huu ambao marehemu alitoa mwishoni mwa miaka ya 1980 na kuzidi kumpa umaarufu mkubwa.

**SWEET MAMA**
Ni ngoma ambayo unaweza kusema ndiyo nembo ya mwanamuziki huyu. Kwenye sherehe mbalimbali za kijamii wakati huo hasa uswahilini ambapo teknolojia muziki wenye maspika makubwa bado haujakuwepo, ziliwekwa redio kaseti na watu kujimwaga kucheza. Wimbo huu ulikuwa haukosi.

**COME ON SAY YOU DO**
Hili ni moja kati ya 'debe' lililopendwa sana na vijana kwenye klabu ambapo walikuwa wakiingia kati na kushindana, kila mmoja akionyesha umahiri wake.

**I'M ACCUSED**
Ni ngoma ambayo ilizidi kumuonyesha Pat Shange ni moja ya wanamuziki wenye heshima kuwa na mfano wa kuigwa Afrika Kusini, huku akizidi pia kujizoelea umaarufu nchini Tanzania.

**MAN OH MAN**
Ngoma hii aliimba kwa ufundi mkubwa akishirikiana na baadhi ya wanamuziki wake wa kike, wakipishana sauti, akiwaimbisha na wao kuitikia.
Huyu ndiye Pat Shange ambaye amefariki kwa COVID-19 Julai 15 na kuacha simanzi kubwa Afrika, ikiwemo Tanzania ambapo vijana wengi za zamani walicheza sana ngoma zake kwa staili ya kuruka majoka.






# Kandakanda: Maliza mabucha, nyama ile ile

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE filamu hii kuna mambo mawili. Moja inaonyesha kuwa kuna baadhi ya viongozi ambao hutumia madaraka yao kuwanyanyasa na kuwaonea raia, badala ya kuwaongoza na kuwasaidia.
Pili inaonyesha kuwa wakati mwingine binadamu ridhika na unachokipata, na si lazima upate vyote kwa sababu ulichonacho na alichonacho mwenzako vyote ni hivyo hivyo. Ukitaka vyote ukusanye inakuwa ni tamaa tu.
Filamu hii inaitwa 'Kandanda'. Ni jina la mfalme mmoja mwenye akili za kipumbavu, ambaye mwisho wake haukuwa mzuri.
Baadhi ya wasanii walioicheza filamu hiyo ni Flora Mvungi, Hashim Kambi, Judith Bwabutaza, Peter Majaliwa, Adumbe na Aisha Maulidi.
Mfalme Kandakanda anapitisha amri himaya yake, msichana yoyote ambaye atavunja ungo ni lazima apelekwe kwake na kukaa kwa muda wa wiki moja kwanza kabla hajapata mume wa kuolewa, au kurudi tena kwenye familia yake.
Sababu ni kwamba eti, anawafundisha jinsi njema ya kuishi na kumtumikia mwanamume akishaolewa. Yaani huyu mfalme anajifanya kungwi wa kiume. Na akawaaminisha watu wa kwenye milki yake kuwa ni amri ya mizimu yao na yoyote asiyetekeleza hivyo, mizimu itakasirika na kuleta maafa. Hivyo familia au binti atakayekataa, atauawa.
Nyuma ya pazia ni kwamba nia ya mfalme ni kuwadhalilisha mabinti hao kwa kuridhisha nafsi yake.
Yaani anataka kila msichana mwenye mume au asiyeolewa kwenye himaya ile, awe tayari ameshampitia.
Baadhi ya mabinti wanauawa kwa kukataa kutekeleza amri hiyo. Anatokea msichana mmoja aitwaye Mwalu. Yeye bada ya kuvunja ungo anakataa kwenda kwa mfalme. Kabla ya kumuua anamfunga.
Kijana mmoja aitwaye Maganzo anakataa kuoa msichana yoyote kijijini hapo kwa madai hawezi kuoa mwanamke ambaye ameshapitia kwa mfalme.
Na yeye ndiye anamuokoa Mwalu na kukimbia naye usiku hadi kwenye himaya nyingine inayoongozwa na malkia. Baada ya simulizi hilo anaahidi kuwasaidia.
Kwa msaada wa malkia huyo, binti yake Nyamaliza na jeshi la himaya hiyo, wanavamia kwenye himaya ya mfalme na kumpa kichapo cha nguvu. Jeshi la mfalme Kandakanda linazidiwa, mwenyewe anauawa na wanakijiji wanarudi kwenye hali ya amani chini ya mfalme mpya, Maganzo.

# Dr Dre kubali yaishe



MKONGWE wa muziki wa Marekani, Dr Dre, ametakiwa kumlipa aliyekuwa mke wake, Nicole Young, dola za marekani 300,000, kama pesa za matunzo kila mwezi.

Mwanamuziki huyo bilionea itambidi kulipa milioni 3.4 kila nusu mwaka kwa mtalaka wake huyo baada ya mahakama kupitisha hukumu ya kuvunja ndoa yao.

Kulingana na mtandao wa Radar, jaji wa mahakama ametoa hukumu hiyo baada ya kufikia mwisho wa usikilizwaji wa pande zote.



## Kanye West arudi Instagram

BAADA ya kukaa nje ya mitandao ya kijamii kwa muda wa miaka miwili, hatimaye rapa Kanye West, amerudi tena kwa kufungua akaunti ya Instagram.

Rapa huyo mwenye ukwasi wa fedha, ameanza kuonekana katika mtandao wa kijamii tangu siku ya Jumanne ya wiki hii ikiwa sambamba na uzinduzi wa Albam yake mpya inayoitwa "Donda."

Mwanamuziki huyo aliposti picha yake akiwa amekaa katika maeneo mbalimbali pamoja na watoto wake North, Saint, Chicago na Psalm.


## Yvonne afunga ndoa kiaina

MWIGIZAJI kutoka Ghana, Yvonne Nelson, imeelezwa amefunga ndoa na mpenzi wake raia ya Italia

Kulingana na ripoti kutoka vyanzo vya karibu, msanii huyo alifunga ndoa hiyo wiki mbili zilizopita, lakini Yvonne mwenyewe hajajitokeza kuzungumzia suala hilo.

Blogu moja nchini humo imefichua taarifa hiyo baada ya kumpa pongezi mwigizaji huo kwa kuingia maisha ya ndoa.





## Runtown amwaga mpenzi wake

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Runtown na mpenzi wake Adut Akech, inadaiwa wamemwagana rasmi baada ya kuishi kwa muda wa mwaka mmoja.

Kuachana kwa mastaa hayo imefahamika hivi karibuni baada ya mrembo huyo kuwasiliana na mashabiki wake katika mtandao wa Instagram.

Mmoja wa mashabiki hao alimuuliza Adut kama yupo singo, na yeye bila ya wasiwasi alijibu kwamba yuko peke yake kwa sasa na jambo hilo ni la kweli.

## Mr Ezi unawapa tabu watu

MWIMBAJI nyota wa Nigeria, Mr Ezi, amekuwa na maisha tofauti kila muda unavyosonga mbele tangu alipoanza kutoka kimapenzi na Temi Otedola.

Mr Ezi sasa amekuwa na maisha ya kula bata, kiasi ambacho mashabiki wake wanahoji kama mtindo huo ni kama anataka kujionyesha kwamba ni tajiri.

Hata hivyo, mwenyewe amewajibu mashabiki hao kwamba hali hiyo ni jambo la kawaida kwake, na siku moja atakuwa mmoja wa watu wakubwa nchini humo.



MAKALA

# WANAHABARI NA RUSHWA NGONO:
# Mdudu aliyeko mtaani kwao, kumnasa mtihani mgumu wanaofaulu 'kiduchu'

- Waathirika: Nusu hawajui, wanaojua hawasemi
- TAMWA: Robo tatu ni matunzo, jinai hawagusi
- LHRC: Kwa ujumla uelewa bado ni shida kubwa

**Na Mary Geofrey**

SHERIA ya Kupambana na Kuzuia Rushwa nchini ina kifungu cha kuzuia rushwa ya ngono, ikianisha kosa kwa mwenye mamlaka kudai au kuomba rushwa ya ngono, kama sharti la ajira, upendeleo, kupandisha cheo, haki au huduma maalum.

Maboresho yaliofanywa na serikali kuhusu sheria hiyo, rushwa ya ngono inatajwa kuwa uhujumu uchumi na adhabu yake inaagukia kifungo cha muda mrefu.

Hata hivyo, rushwa ya ngono na unyanyasaji wake imebaki binafsi zaidi, pia vyombo vyenye mamlaka penye matukio viko kimya kuhusu udhibiti au hatua dhidi ya wahusika.

Nipashe ilichunguza katika vyombo vya habari kufahamu sera, kanuni na taratibu za udhibiti na kama vina kiongozi maalum wa kupokea malalamiko ya unyanyasaji kingono dhidi ya walalamikaji.

Wanahabari wanakiri vitendo hivyo, pia wanaona kuna umuhimu wa kuwa na sehemu ya kuripoti.

Mhariri wa Habari wa gazeti la serikali la Habari Leo, Stellah Nyemenohi, anasema unyanyasaji kingono halijawaathiri ofisi yao, ingawa anakiri kuvisikia katika vyumba vingine vya habari.

Anataja sababu ya ushindi wa kwa matukio hayo, ni zao la mifumo ya uongozi, pia utumishi wa umma akitetea ofisini kwake kuna kuheshimiana kwa rika na jinsia, hali inayofuta unyanyasaji wa kingono.

Stellah anasema, huenda kukawepo mtu mmoja mmoja, lakini hayajamuathiri mhusika na ndio maana hayasikiki.

"Misingi ya ofisi yetu na uongozi nadhani ni kama familia inayokuwa na maadili hata akija mgeni mwenye tabia mbaya hawezi kuonyesha au kuendeleza, kwa sababu ya misingi aliyoikuta," alisema Stellah.

Aliyekuwa Mhariri wa Habari wa gazeti la michezo Champion, John Haramba, anasema matukio hayo yapo, lakini hayachukuliwi uzito.

Kwa nafasi yake uhariri wa habari, amewahi kuyasikia yakizungumzwa, lakini hayapewi kipaumbele kwenye utendaji kazi, ikibaki suala binafsi.

Pia, anasema hajawahi kusikia kuwapo dawati, ofisi au mtu anayepelekewa malalamiko ya unyanyasaji wa ngono katika chombo hicho cha habari.

Haramba, ambaye sasa ni Mhariri Mkuu wa Radio Times, anashauri kuwapo mfumo madhubuti kuzuia unayanyasaji kingoni katika vyombo vya habari.

"Tukisema kuwe na dawati au mtu ambaye ataelezwa matukio kama hayo, anaweza asifikishe kwa mhusika au hatua zisichukuliwe," anaeleza.

Nashauri kuwapo sanduku la maoni, litakalosaidia kufikisha maoni bila anayelalamikiwa kumtambua anayemtaja.

Haramba anasema, kuna umuhimu wa taratibu madhubuti kuwezesha waandishi wa habari kuripoti matukio hayo, endapo yanatokea kusaidia kuweka usawa kijinsia na kumaliza usumbufu.

Anasema, kwa wanaokutana na usumbufu huo inakuwa fursa muhimu kuripoti, ili hatua zichukuliwe kudhibiti tabia.

Pia, mwandishi wa habari ambaye hakutaka jina lake liandikwe kutoka kituo kimoja cha redio (tunalihifadhi), anasema kwao hakuna dawati la kuripoti matukio.

Hata hivyo, anaona umuhimu wa dawati, kwani yapo mambo yanawatesa wanahabari na inawapa fursa wakajieleza kwa uhuru na hatua zikachukuliwa.

Anasema ofisi ya Ofisa Rasilimaliwatu ndio inayohusika na kusikiliza matatizo na kero za wafanyakazi, lakini haina meno, akifafanua:

"Meneja Rasilimali Watu ni bosi, unavyompelekea kesi kubwa, bosi mwenzie amefanya tukio fulani inakuwa ngumu kilichukulia kwa uzito na zaidi ili asionekane kuwa ni 'mnoko' kwa hiyo wanamaliza kesi," anasema.

Mwandishi wa habari wa Radio Maria, Happiness Mlewa, anasema ofisi ina huduma ya kuwasikiliza shida zao.

"Tumemteua kiongozi wetu mwanamke ambaye ikitokea mwenzetu amekutwa na changamoto yoyote ataenda kutoa taarifa kwake na tumefanya hivyo bila kushirikisha wengine," anasema Happiness.

Anafafanua umuhimu wa madawati au ofisi maalum ya malalamiko, ili kuwasaidia vijana wanaoingia kwenye fani wakapokutana na magumu hayo wasikate tamaa.

Nipashe imezungumza na Msimamizi Mkuu wa Vipindi wa Redio Maria, Agness Shayo, mpokeaji malalamiko ya wanawake wanaonyanyasika kingono, anayekiri kupokea dai moja mwaka 2019 na mhusika aliitwa na mamlaka ya ofisi, akaonywa.

"Jambo hilo hakulirudia tena na hata hivyo kwa sasa siyo mfanyakazi tena wa Radio Maria," anasema Agness.

Anasema sababu ya mafanikio kuwapo matukio machache, inatokana na msingi wa chombo cha habari, ambacho ni cha kanisa, Agness akimsifu kiongozi wao wa juu amekuwa mstari wa mbele kuwatetea na kuwapa fursa kufikia malengo yao.

"Mwaka jana katika kusherehea Siku ya Wanawake, tuliamua kumpa zawadi kwa sababu amekuwa kiongozi bora anayejali na kututetea zaidi wanawake," anasema Agnes.

**KUTOKA TAMWA?**

Mratibu wa Kituo cha Usuluhushi (CRC) cha Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania(TAMWA), Gladness Munuo, anasema kwa miezi mitatu, wanapokea madai 100 ya ukatili kijinsia na asilimia 80 zinahusu matunzo, zilizobaki ndizo ukatili kingono.



Mratibu wa Kituo cha Usuluhushi (CRC) cha Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA), Gladness Munuo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Anasema, katika kesi hizo kinamama malalamiko yao mengi ni ajenda tofauti na ukatili kijinsia kama vile unyanyasaji kingono.

"Wanahabari wanajificha kuhusu kuripoti matukio ya unyanyasaji wa kingono," anasisitiza Gladness.

**UTAFITI WA LHRC**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kinasema wanawake na wasichana wengi wanakatiliwa kijinsia na hawafahamu mifumo ya kuwapa haki, pia namna ya kuwasaidia, wanapokumbana na madhila ya kikatili.



Wanahabari wakiwa katika mafunzo ya taaluma yao jijini Dodoma

LHRC imebaini mara nyingi msuguano aina hiyo huishia katika vikao vya kifamilia, ili yasifike mbali.

Utafiti wa Afya Tanzania wa Mwaka 2015/16 unaeleza asilimia tisa ya wanawake wanaripoti polisi matukio ya kunyanyaswa polisi na asilimia 54 kati yao ndio wanaopata msaada katika vyombo vya dola na wanaobaki husuluhisha kifamilia, hali inayowaathiri sana wanawake wanaokatiliwa.

**WIZARA YA AFYA**

Mwongozo wa Uratibu wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wa miaka 2017/18 hadi mwaka uliopo wa fedha, uliotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, unasema serikali na wadau wamekuwa wakifanya juhudi kukabiliana na ukatili nchini kupitia sera, sheria, kanuni, miongozo na mipango ya kisekta.

Inazitaja kuwa sera za: Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Maendeleo ya Mtoto (2008) na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Kanuni zake ndizo zilianzisha Dawati la Jinsia kwenye wizara zote na mifumo ya ulinzi wa mtoto katika halmashauri 63 kitaifa.

Pia, kulianzishwa Dawati la Jinsia kwenye vituo vya polisi na kuanzishwa mahakama za kusimamia kesi za watoto katika halmashauri 131.

MTAKUWWA inawajibika kuhakikisha utekelezaji Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto na kutoa huduma kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi,

Ni hatua inayoendana na mikataba ya kikanda na kimataifa ya haki na ustawi wa wanawake na watoto, sera, sheria na miongozo serikalini.

**RIPOTI YA UNFPA**

Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) ya Aprili 14 mwaka huu, inakadiria nusu ya wanawake katika nchi 57 zinazoendelea wananyimwa haki za kuamua kuhusu miili yao, ikiwamo tendo la ndoa.

Ripoti hiyo kwa mara ya kwanza imejikita katika dhana uhuru wa mwili, nguvu na umuhimu wa kuamua kuhusu mwili bila ya hofu, ukatili au mtu mwingine, pia kukosekana haki katika ufungaji kizazi, kupimwa bikira na ukeketaji. UNFPA inaeleza kukosa uhuru huo una athari kubwa kwa kinamama

Kupitia ripoti hiyo, UNFPA imepima nguvu za wanawake kuamua kuhusu miili yao na kiwango sheria za nchi zinaunga mkono au zinaingilia haki ya mwanamke kuamuaa.

## 'DEZO' YA MIEZI MITATU...

# Wateja simu watiwa kiwewe na dakika bure kwa saa za asubuhi

## ●Nao waugeuza mtaji wa mawasiliano kazini

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI sasa inatajwa 'simu ndio mpango mzima.' Mawasiliano, benki ndogo, saa na ulingo wa kujiliwaza.

Hapo ndio inazaa sababu hata katika kila mabadiliko ya gharama za kodi, ilivyozaa taharuki kwa umma.

Pia, katika eno hilo la 'mabando; hapo ndiko kuna starehe na michezo ya kujiliwaza hata mtu anapopumzika anaangukia kurejea simu yake imliwaze kwa namna nyingi.

Wakati watu sasa wametawaliwa na makuu ya kinachojiri kwenye kodi za bando zao na huduma nyinginezo, kwa sasa watoaji huduma kila kukicha nao wanakumbana na namna gani wanaibuka upya kuishinda soko kuwa na sura inayoshabiliana ya watumiaji.

Hapo ndipo wadau wamechukua fursa kuibuka na mfumo wanaojigamba nao unampa kifua mhusika mkuu ambaye ni mtumiaji wa ngazi ya chini, ananufaika zaidi hasa kwa gharama na ikilenga maslahi yake.

Kwa jina imebatizwa kuwa 'Bonasi ya Asubuhi' na katika uzinduzi wa huduma hiyo mpya Mnamo Juni 15, mwaka huu, Kaimu Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Tigo, David Umoh, anajigamba:

"Daima tunatafuta njia za ubunifu za kuwazawadia wateja wetu wenye kazi na kuwafurahisha, kampeni hii inatoa fursa nzuri ya kuungana na wateja wote tuliokuwa nao kwa muda mrefu.

"Tunaamini kuwa mipango mingi hufanywa mapema asubuhi na kwa kuwa tuna nia ya kukidhi mahitaji ya wateja wetu kote nchini. Kampeni hii inawapa fursa watu wanaoamka



Matumizi ya simu na mitandao yake yamechachamaa kila mahali. kwa namna tofauti, ikiwamo hivi sasa ni zama mpya za 'Cha Asubuhi' kutoka mtandao wa Tigo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

mapema na wale ambao wanapendelea kupanga shughuli zao za kila siku kuanzia asubuhi," anaeleza.

Kampuni ya Tigo ilizindua kampeni mpya ya siku 90 ya bonasi ya 'Cha Asubuhi' ili kila mteja anayenunua kifurushi Cha kila siku au wiki anufaike.

Umoh anasema ni miaka mingi wamekuwa wakianzisha ubunifu wa mifumo na mitandao ya simu yanayokidhi mahitaji tena kwa lugha ya nchini Kiswahili, ikijumuisha vifurushi na 'facebook' za bure, na simu za Kiswahili na vifurushi vyake.

"Mipango yetu ni kuhakikisha tunaondoa vizuizi kwa wateja wetu kwa ajili ya kufanya mawasiliano ya muhimu kupitia kampeni mpya ya 'Cha Asubuhi,'" anasema kwamba kuna kundi kubwa la wateja wanaozidi milioni 10 wa Tigo watanufaika na kupiga simu bure pindi wakiamka.

Mbali na hiyo, watanufaika na programu za 'kuperuzi' mtandao pasipo shaka kwa maongezi ya simu zao. Anaendelea: "Hii inadhihirisha juhudi zetu katika kuwa fursa inayowapa wateja wetu huduma bora."

Umoh anaongeza kuwa ni kampeni itakayoendelea kwa siku 90 na walengwa ni wateja wote wa Tigo, wanufaike na jasho la pesa na uanachama wao.



**WANUFAIKA WANENA**

Dereva wa Bajaj wa eneo la Kituo cha Mabasi cha Mbezi, Juma Iddy, ambaye hafichi tabasamu lake 'anafunguka; kuwa ananufaika na bonasi ya 'Cha Asubuhi' ya Tigo, kutokana na kumrahishia mawasiliano na wateja wake kila siku inapoanzia asubuhi.

Anasema wateja wake wengi wanafanya shughuli zao za kila siku kuanzia majira ya alfajiri, hivyo amekuwa akiwasiliana nao kwa kupitia mtandao wa Tigo bila kuwa na kizuizi chochote.

Iddy anaishukuru programu hiyo kutokana na kuwa wabunifu, kila siku wamekuwa mstari wa mbele kuwajali wateja wao na kusikiliza nini wanahitaji.

"Mimi kawaida najiunga kifurushi cha wiki cha muda wa maongezi. Hapo ndio nikagundua kuna bonasi ya muda wa maongezi, kwa jina la 'Cha Asubuhi'.

"Nimekuwa nikitumia muda wangu wa maongezi wa bonasi kila siku kwa ajili ya kuwasiliana na wateja wangu hasa wale wanaofanya safari zao kutoka eneo moja kwenda jingine.

"Ninawashukuru Tigo wamekuwa wabunifu kila wakati, ikiwa ni pamoja na kuturahisishia maisha kila siku na tutaendelea kuwa nao kwa muda wote," anatamka kwa bashasha.

Mfanyabiashara wa chakula wa eneo la Buza, jijini Dar es Salaam, Sarah Seleman, anasema huwa anatumia bonasi ya 'Cha Asubuhi' kuwasiliana na wateja wake wa chakula.

Sarah anajitambulisha kuwa ni mfanyabiashara wa chakula anayejivunia kuwasiliana na wateja wake wote kuanzia asubuhi kwa ajili ya kuweka 'oda' ya chakula mapema.

Kupitia bonasi ya 'Cha Asubuhi' huwa anawasiliana na wateja wake na kupokea oda mbalimbali, hivyo anasema anafurahia kwa kiasi kikubwa kutumia mtandao huo.

"Cha Asubuhi na Tigo ndio 'habari ya mjini', kwani bila cha asubuhi mambo huwa hayaendi, nimekuwa nikitumia bonasi zangu baada ya kujiunga kifurushi cha siku.

"Nasubiri muda wa saa kumi na mbili hadi saa tatu kesho yake kuwasiliana na wateja wangu na kuchukua oda za chakula kwani ninapata dakika kemkem kila siku," anasema.

Muuza 'movie' wa Buguruni Sheli, Dar es Salaam Shabani Hassan, anasema amekuwa akitumia bonasi hiyo tajwa kupakua filamu mpya za kuwasambazia wateja wake.

Anasema, awali alikuwa akipata shida kupakua filamu kutoka kwenye mitandao mbalimbali lakini kupitia bonasi 'Cha Asubuhi; wamemrahishia kazi yake na kwamba kwa sasa amekuwa akienda sawa na wateja wake kila siku.

"Awali nilikuwa napata shida kupakua filamu mpya kutoka katika mitandao, lakini baada ya kujiunga kifurushi cha intaneti cha mwezi," anasema na kutaja bonasi imemsaidia kwa kiasi kikubwa.

Mnamo Juni 15, mwaka huu, kampuni ya Tigo ilizindua kampeni mpya ya siku 90 ya bonasi ya 'Cha Asubuhi' katika kampeni hiyo mpya kwa kila mteja anayenunua kifurushi 'Cha kila siku," kila wiki.

Ni bonasi ya dakika za bure kupiga 'Tigo kwa Tigo kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa tatu3 na mteja wa kifurushi cha kila siku atapata bonasi ya dakika 10 hadi 'mb; 10, wakati mteja wa kifurushi cha kila wiki atapokea dakika 70 hadi mb 700; huku mteja wa kifurushi cha kila mwezi anapata dakika 300 na 'GB 3.

Umoh anasema wateja wote wanatakiwa kujisajili kwenye kifurushi cha chaguo lao kupitia menyu na 'App' maalum zenye haki ya kutumika kati ya saa 12 asubuhi hadi saa tatu asubuhi kila siku bila malipo.

# Wananchi wamzika rais Jovenel Moïse

**Port-au-Prince,** HAITI

RAIS Jovenel Moïse wa Haiti, aliyeuawa mapema mwezi huu, baada ya kundi la watu wenye silaha kuvamia makazi yake binafsi huko Port-au-Prince, amezikwa.

Mazishi ya Jovenel Moïse yalifanyika jana katika mji wa Cap, Haiti, kwa mujibu wa taarifa ya serikali.

Polisi ya Haiti inawashikilia karibu watu 20, ikiwa ni pamoja na wanajeshi kadhaa wa zamani wa Colombia wanaotuhumiwa kuwa sehemu ya kundi la watu waliokuja kumuua rais Moïse, bado uchunguzi unaendelea.

Polisi ya Colombia, ambayo pia inafanya uchunguzi kuhusiana na mauaji hayo, siku ya jana ilisema kwamba ofisa wa zamani wa wizara ya sheria ya Haiti, Joseph Felix Badio, aliamuru mamluki wawili wa Colombia wamuue rais Jovenel Moïse.

Vurugu zilizuka kabla ya mazishi na kulishuhudiwa machafuko alhamisi wiki hii katika mji wa Kaskazini Haiti, wa Cap-Haitien wakati waandamanaji walipoweka vizuizi barabarani wakipinga mauaji ya rais huyo.

Polisi waliokwenda kwenye mji huo kwa ajili ya kusaidia kusimamia mazishi ya rais huyo walikutana na waandamanaji ambao ni wafuasi wa kiongozi huyo, wanawataja polisi kuhusika na mauaji kwenye makazi ya rais Julai 7.

Mtu mmoja amekufa kwenye vurugu hizo, aidha Marekani imemtangaza Daniel Foote kuwa mjumbe maalumu atakayesaidia kuratibu misaada ya Marekani nchini Haiti pamoja na juhudi za kupatikana amani ya kudumu na uchaguzi.

Moise aliyekuwa na umri wa miaka 53, alitawala kwa amri ya rais kwa zaidi ya miaka miwili, baada ya nchi hiyo kushindwa kufanya uchaguzi, hatua iliyopelekea kuvunjwa bunge.

RFI



# Majaji Mahakama Kuu Kenya watuhumiwa kwa ufisadi

**Nairobi,** KENYA

MAJAJI wawili wa Mahakama Kuu Kenya, Aggrey Muchelule na Said Juma Chitembwe Alhamis wamekamatwa na maofisa wa idara ya upelelezi wa makosa ya jinai kwa madai ya kula rushwa kutokana na kesi walizosikiliza awali jijini Nairobi.

Wawili hao walihojiwa kwa zaidi ya saa mbili na kisha kuachiliwa baadaye, ingawa wakili wao, Danstan Omari anaeleza kuwa ni mwendelezo wa hatua za serikali kuminya uhuru wa idara ya mahakama. Wengine waliofikishwa katika makao hayo kuandikisha taarifa ni pamoja na makarani na madereva wanaofanya kazi kwenye ofisi za majaji zao.

Muchelule ni mojawapo wa majaji waliokosa kuteuliwa kwenye mahakama ya rufaa na Rais Uhuru Kenyatta kwa madai ya kuwa na dosari za maadili.

Yeye pia ni miongoni mwa majaji sita kati ya 40 ambao Kenyatta hakuwapandisha vyeo alipofanya uteuzi huo, Juni, mwaka huu.

Wengine walioachwa nje ni majaji Prof. Joel Ngugi na George Odunga. Japo vyombo vya habari vya Kenya vinanukuu maofisa wa upelelezi kuwa kuna masuala mazito wanayochunguza dhidi ya majaji hao wawili, wakili wao Danstan Omari anadai kuwa, kuna masuala yasiyoeleweka.

Rais Kenyatta amekuwa akikabiliwa na shutma chungu nzima kwa kuteua majaji 34 na kuwaacha wengine sita bila kuweka wazi sababu za kufanya hivyo, ikionekana kama uminyaji wa uhuru wa idara ya mahakama.

Muungano wa mahakimu tayari umeeleza kuwa Kenyatta hana uwezo kisheria wa kuchagua baadhi ya majaji huku akiwaacha wengine.

Baraza la Wanasheria Kenya (LSK)kupitia rais wake Nelson Havi, limeeleza kuwa hatua ya makachero kuwakamata na kuwaacha bila kuwafungulia mashtaka majaji hao, ni kuhujumu na kuminya uhuru wa idara ya mahakama.

VOA



Watoto wakicheza nje ya makazi yao katika siku ya Sikukuu ya Eid al-Adha Kaskazini mwa Ukingo wa Gaza, mjini Beit Hanoun, juzi. **PICHA: XINHUA**

# Dubai yabuni mvua feki kukabiliana na joto kali

**UAE,** DUBAI

ILI kuepuka madhara ya joto Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), Dubai kupitia kitengo cha hali ya hewa kimebuni teknolojia inayoweza kupunguza hali ya joto, na kutengeneza mvua feki.

Dubai inapitia kipindi kigumu cha hali mbaya joto kali, nchi hiyo iliyopo ndani ya UAE linashuhudia joto kupindukia hadi nyuzijoto 50.

Inakadiriwa joto limekwishaua zaidi ya watu 500 Canada na Dubai, na kuhatarisha maisha ya watu zaidi ya milioni tatu, wanaoishi katika mji huo.

Hivi karibuni nchini Canada zaidi ya watu 500 waliripotiwa kufariki dunia kwa sababu ya joto kali.

Kituo cha hali ya hewa Dubai, kupitia tovuti yake, wiki hii kilichapisha video kupitia mtandao wake wa twitter ikionyesha mvua hiyo kubwa kiasi iliyokuwa inanyesha kwenye maeneo kadhaa, huku watu wakiendelea na maisha yao ya kawaida na magari yakionekana yakipita kwenye barabara kubwa zenye mvua.

Zilitumwa ndege zisizo na rubani kwenye mawingu yaliyo usawa wa kando kidogo ya mji wa Dubai ili kutekeleza teknolojia hiyo, ambayo imeanza sasa kufanyiwa majaribio sasa.

Kwa mujibu wa taarifa za kitengo cha hali ya hewa cha UAE ni kwamba, zimetengenezwa ndege ndogo maalumu zisizo na rubani (Drones), ambazo zimewekewa nguvu maalumu ya umeme.

Ndege hizi zinatumwa angani kwenye mawingu zikifika huko zinaruhusu umeme ambao huleta mshituko ama kupiga shoti mawingu na kuyasukuma mawingu hayo kubadili muundo wake.

Kubadilika huko kunasababisha unyevu na maji ambayo yakidondoka ardhini yanakuwa mvua ambayo haina tofauti yoyote na mvua iliyozoeleka.

Mtaalam mbobezi anayefanya kazi kwenye mradi huo wa mvua feki Prof Maarten Ambaum, aliwahi kunukuliwa na BBC kuhusu mradi huo na miradi mingine ya mvua feki, hasa wakati huu nchi hiyo ikikumbwa na joto.

"Nchi hii ina mawingu mengi sana, kwa hiyo mpango uliopo ni kusukuma mawingu haya ya matone ya maji yaweze kushikamana kama nywele kavu wakati yatakapokutana na umeme.

"Matone haya yakiungana na kuwa makubwa, yanadondoka, yanapodondoka yanakuwa mvua." alisema mtaalamu huyo.

Alya Al-Mazroui, Mkurugenzi wa Kitengo cha Masuala ya Utafiti wa Mpango wa Mvua za ziada, alisema wakati wa majaribio ya mpango ama teknolojia hiyo, ni ndege kupaa kwenye anga la chini na kurusha umeme huo kwenye mawingu na kuleta mvua.

UAE hasa eneo la Dubai hupata mvua chache sana kwa mwaka, kiasi cha 100 milimita pekee, kiwango ambacho ni kidogo mno, kutokana na mazingira na hali yake ya ukame.

Kuongezeka huwa ni jambo la kawaida Dubai, kiasi cha kuufanya mji huo kuwa na changamoto, unaotajwa kuwa miongoni mwa miji ya kitalii inayopendwa duniani.

Kwa sasa mamlaka za hali ya hewa zinapambana kuongeza kiwango zaidi cha mvua, ili kupunguza joto.

BBC

# Mfumo warahisisha vibali kazi saa 24

Na Joseph Mwendapole

MFUMO mpya wa kuomba vibali vya kazi kidijitali umewezesha wawekezaji kupata ndani ya saa 24.

Kamishana wa Kazi Ofisi ya Waziri Mkuu, Brigedia Jenerali Francis Mbindi, alisema juzi wakati akiwasilisha mada kwenye mkutano ulioandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI) na wawekezaji kuhusu vibali vya kazi.

Alisema mfumo huo ambao umeondoa urasimu na kupunguza siku za kusubiri vibali vya kazi, ulianza kutumika mwezi Aprili, mwaka huu na unatarajiwa kuzinduliwa rasmi mwezi Agosti.

Alisema mfumo huo umekuwa mwarobaini wa tatizo la upatikanaji wa vibali vya kazi ambavyo kwa mfumo wa awali iliwalazimu wawekezaji kusafiri umbali mrefu kwenda kwenye Idara ya Kazi na kupoteza fedha na muda barabarani.

Alisema kwa mfumo wa sasa mtu halazimiki kwenda kwenye ofisi yoyote ya serikali kwa kuwa anaweza kujaza fomu kidijitali akiwa popote duniani na kibali chake kikaanza kushughulikiwa akiwa bado yuko nje ya nchi na hakuna tena matumizi ya makaratasi.

Brigedia Jenerali Mbindi alisema ingawa sheria ya kuratibu ajira za wageni namba (1) ya mwaka 2015 inamtaka Kamishna wa Kazi kushughulikia vibali vya kazi ndani ya siku 14, lakini vilikuwa vikichukua muda mrefu kuvipata kutokana na mlolongo wa urasimu na changamoto zilizokuwapo.

Alisema ili kupata kibali cha kazi kwa mfumo wa zamani kulikuwa na hatua 33 za kupitia, lakini baada ya kuanza mfumo huo mpya sasa hatua hizo zimepungua kutoka 33 hadi saba.

"Kwa sasa kama mwombaji atajaza fomu kwenye mfumo na nyaraka zake zote zikawa zimekamilika basi ana uhakika kibali chake cha kazi kitatoka ndani ya saa 24, tumepunguza kero na malalamiko ya wawekezaji ambao walisumbuka sana," alisema.

Alisema mfumo huo mpya umeunganishwa na wa Idara ya Uhamiaji inayoshughulikia vibali vya ukaazi na mwombaji atajaza fomu moja kwa njia ya mtandao ambayo itahusisha maombi ya kibali cha kazi na cha ukaazi.

Alisema mwisho wa siku mwombaji atapata kadi yenye taarifa zote za kibali cha kazi na kile cha ukaazi ambayo inafanana na kadi ya benki itakayomwezesha kuibebaba popote tofauti na mfumo wa zamani wa kujaza makaratasi mengi.

"Muda umepungua sana na gharama za kushughulikia vibali vya maombi kwasababu waombaji walilazimika kutufuata tulipo na hata serikali tulikuwa tunatumia karatasi nyingi sana kushughulikia vibali, lakini kwa mtandao tumeokoa matumizi ya karatasi ambazo zilikuwa zikitugharimu sana," alisema.

Alisema mfumo huo umeunganishwa na taasisi mbalimbali za serikali kama mfumo wa malipo ya serikali kielektroniki, Wakala wa Usajili wa Leseni za Biashara (BRELA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na kuwawezesha kupata taarifa mbalimbali za mwombaji tofauti na awali walipomtaka kuzipeleka mwenyewe Idara ya Kazi anapowasilisha maombi.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Chinokole wilayani Ruangwa mkoani Lindi jana. **PICHA: OWM**

## Mwinyi apongeza utayari wa Blair

Na Mwandishi Maalum

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepongeza utayari wa Waziri Mkuu mstaafu wa Uingereza, Tony Blair wa kuiunga mkono Zanzibar kupitia taasisi yake ya Mabadiliko Ulimwenguni (Tony Blair Institute for Global Change).

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu jijini Zanzibar alipokutana na kufanya mazungumzo na Blair ambaye alikuwa Zanzibar kwa ziara maalum ya siku moja.

Dk. Mwinyi alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kushirikiana na Taasisi ya Blair ili kuihakikisha azma iliyokusudiwa inafikiwa.

Rais Mwinyi alitumia fursa hiyo kumpongeza Blair kwa kufanya ziara Zanzibar na kubadilishana mawazo katika mustakbali mzima wa kuiletea maendeleo Zanzibar.

Alisema ana matumaini makubwa kuwa mazungumzo baina yao yatakuwa chachu ya maendeleo hasa ikizingatiwa kwamba Blair ni kiongozi mwenye mwenye uzoefu mkubwa wa uongozi duniani.

Alitoa shukrani zake kwa Waziri Mkuu mstaafu huyo kwa kueleza nia yake njema ya kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia taasisi yake.

Blair alimweleza Rais Dk. Mwinyi kwamba taasisi yake iko tayari kushirikiana na kuiunga mkono Zanzibar katika kutafuta njia bora za kupanga mikakati ya kutekeleza mipango ya maendeleo.

Alisema timu yake kutoka taasisi anayoiongoza iko tayari kuja na kukaa na wataalamu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuanza taratibu hizo za kuhakikisha utekelezaji wa mazungumzo hayo unafanyika ikiwa ni pamoja na kusaidia vipaumbele vya serikali.

Alisema taasisi yake inathamini juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Mwinyi na kuahidi watakuwa bega kwa bega katika kuhakikisha inashiriki ipasavyo kufikia malengo yaliyowekwa na serikali.

Aliyasifu mazingira mazuri ya Zanzibar na kuahidi kurudi tena kuitembelea zaidi Zanzibar mara baada ya kumazika kwa janga la corona ambalo limemnyima fursa ya kutekeleza azma yake hiyo kwa sasa.

## CCM Pwani yampongeza Samia kusikia kilio

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Pwani, imempongeza mwenyekiti wa chama hicho taifa ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu kwa namna anavyozitafutia ufumbuzi kero za wananchi ikiwamo makato kwenye miamala ya simu.

Akiongea na waandishi wa habari jana mjini hapa, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani, Ramadhani Maneno alisema kitendo cha rais kuanza kutoa maelekezo kwa mawaziri wenye dhamana kukaa na wadau ameonyesha wazi anavyoguswa na kero za wananchi anaowaongoza.

"Tumekuja hapa kuunga mkono kauli ya Mwenyekiti wetu Rais Samia Suluhu ya kusikia kilio cha wananchi mahusus kwenye masuala ya makato kwenye miamala ya simu alipotoa maelekezo kwa mawaziri wenye dhamana kukaa na wadau hii imetufanya leo kuwa hapa na kumpa pongezi zake," alisema.

Alisema chama kimemkabidhi ilani ambayo ndani kuna maagizo ya mambo mbalimbali ikiwamo kutatua kero za wananchi na kwa anachokifanya anatekeleza ilani iliyomweka madarakani.

Alisema CCM Mkoa wa Pwani inaamini hatoishia kwenye mambo ya miamala pekee bali ataendelea kushughulikia kero nyingine zinazoleta malalamiko kwa wananchi.

Baadhi ya wakazi wa Mailimoja Kibaha wameomba rais kulifanyia kazi suala hilo kwa haraka kwa kuwa imekuwa kikwazo kuwatumia fedha ndugu zao ambao wako mbali.

Athumani Ally, mkazi wa Mailimoja alisema makato kwenye simu ni maumivu makubwa hali iliyomsababishia kushindwa kutuma fedha kwa mama yeke ambaye anaishi Mvomevo kutokana na kiasi kidogo alicho nacho.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Mwanaume anaweza kwenda peke yake, lakini hawezi kumaliza na kuondoka akiwa yake. Atapata mpenzi hapo hapo. Au atakaa na muda si mrefu atakuja mpenzi wake walioahidiana naye.

Ukiona mwanaume amekwenda baa kuanzia mwanzo hadi mwisho. Haonekani kuwa na haja hata ya mwanamke. Mawili. ana 'stresi', au kuna kitu amefauta hapo, na hapo wale watu wa intelenjia au siku hizi wanasema kuwa 'waliosomea Cuba', watakuwa wana wasiwasi naye.

Tom alilifahamu hilo. Alijua kama kuna mtu mwenye ujuzi huo anaweza kuwa na shaka naye. Alimwita mhudumu mmoja na kuongea naye kwa dakika kadhaa. Dakika tano baadaye alikuja n msichana mwingine.

"Kaka nimekuletea huyu. Ni mhudumu wa baa hii, ila leo yuko 'ofu', amekuja kuleta pesa ya mchezo." Mhudumu alimwambia Tom, akamgeukia mwenzake.

"Tedi huyu mgeni ameomba kampani, hana mtu, kwa hiyo kuwa naye, usiniangushe."

Tedi alikaa kwenye siti ya pili kutoka kwa Tom. Sasa walionekana kama wapenzi kamili. na hilo ndilo alilihitaji. Nao waliagiza viywaji.

Macho ya Tom alishuhudia jamaa yule akimkumbatia na kumpiga mabusu mkewe Farida. Tom aliuma meno. Alitaka kuinuka na kwenda kumshindilia makonde. Alisita. Kuna kitu kilimwambia "Vumilia, kwani kazi haijakamilika." Kwa hasira na yeye akamkumbatia Tedi na kumbusu. Naye alirudisha. Tedi hakujua nini kinaendelea. Alidhani ni mahaba tu aliyonayo mwanaume huyo kwake. Mabusu aliyopigwa na Tedi yalikuwa dawa kwa Tom. Alishusha presha na kuhema kwa nguvu.

***************************

Ilikuwa ni siku ngumu kwa Tom. Kwa macho yake alishuhudia jamaa akiinuka, akiwa amemshika mkono mkewe. Baadaye alimkamata kiuno. Kidogo nguvu zimwishie na kudondoka chini. Alijikaza mtoto wa kiume. Maji ameyavulia nguo, ilibidi ayaoge.

Ilifika wakati hata Tedi alimshtukia mpenzi wake akiwaangalia zaidi watu wale waliokuwa kwenye meza.

"We umekolea sana na yule dada eee." Alisema kwa namna ya ukali kidogo iliyomshtua Tom kwenye mawazo mazito.




**Macho makubwa malegevu, yalibeba taswira kuwa yapo kwa binadamu anayeweza kuyatumia kikamilifu.**

"Nini?"

"Nini nini, wewe unamwangalia sana yule dada na yule mpenzi wake, unanichefua. Sasa umeniitia nini hapa? Unawafahamu?" Aliuliza baamedi Tedi.

"Hapana mpenzi, kuna mmoja kama namfananisha hivi." Alijibu.

"Nani kati ya wale?"

"Nitakwambia baadaye. Tuondoke." Aliamuru Tom.

Na hii ni baada ya mkewe Farida na mtu aliyekuja naye akionekana kabisa kuwa ni mpenzi wake kuondoka.

"Tunakwenda wapi sasa?"

"Kwangu."

"Nyumbani kwako? Huna mke?"

"Hapana, ni kwenye hoteli nilikofikia."

"Kumbe wewe siyo wa hapa Morogoro."

"Ndiyo. Mimi natoka Dar."

Walipofika waliweka mezani chakula walichochukua kwenye baa ya Mwenda na kuanza kuteketeza viazi vya kukaanga na kuviadhibu vipande vya kuku wa kuoka.

Tayari Tom alikuwa ameshaoga na akili yake kuanza kutulia kutokana na tukio alilokutana nalo.

Ilikuwa ni kama anaota ndoto moja mbaya ambayo hajawahi kuota maishani mwake.

Sasa alipata muda wa kumuangalia kwa makini Tedi. Akamshangaa. Kumbe alikuwa hapati muda wa kumuona vizuri kutokana na akili yake yote kuwa kwa Farida.

"Kwa nini ameamua kufanya kazi ya hii huyu?" Alijiuliza.

Ni mmoja wa wasichana wazuri ambao wamewahi kuwaona maishani. Ni mzuri hasa, tena wa asili.

Tena ilionekana kabisa alikuwa na maisha magumu. Kama angekuwa na maisha bora, angetoka kwenye familia ya kitajiri.

"Kama angepata malisho bora huyu ingekuwaje?" Bado kichwa cha Tom kilizidi kujiuliza maswali

Kichwa chake cha mviringo ilibeba midomo mipana yenye kumvutia kila anayemuona.

Macho makubwa malegevu, yalibeba taswira kuwa yapo kwa binadamu anayeweza kuyatumia kikamilifu.

Pua ndogo ya mchongoko, ilizidi kumfanya avutie zaidi. Kichwa chake kilibeba nywele ambazo alizisuka kwa mtindo wa yeboyebo.

"Tedi?" Kwa mara ya kwanza Tom aliita jina lake. Awali alilisikia kwa mwenzake aliyekuwa akihudumia kwenye baa.

Tedi alishtuka kidogo, kwani hakutegemea uitaji ule. Ulikuwa ni wa utulivu wa hali ya juu tena kwa mtu ambaye anamthamini.

Siku zote Tedi alijiona ni mwanamke asiyefaa kwenye jamii. Mwanamke ambaye jamii imemtenga. tayari alishajiweka kwenye kundi la wanawake ambao kazi yao ni kuwafurahisha wanaume. Nao wakishafurahi malipo yao ni kuwadhalilisha utu wao, kuwadhihaki na kuwatisha.

"Abee." Aliitikia kwa utulivu.

"Umeanza lini kufanya kazi hii?"

"Ipi? Hii ya kuuza baa?"

"Ndiyo."

Tedi alizidi kupigwa na mshangao. Hakuna mwanaume yoyote aliyewahi kumuuliza swali hilo. Wanaume wote waliomtaka kimapenzi wao walichokuwa wakitaka ni kukidhi haja zao tu basi.

"Mwaka wa pili huu sasa." Alijibu huku akijaribu kumtazama Tom usoni na kumuona kama mtu mwenye mawazo mengi.

"Kwa nini ulichagua kazi hii na si nyingine?"

Kwanza Tedi alitaka kukasirika. Kwa sababu kazi anayoifanya inanasibishwa na uhuni wakati si kweli.

Uhuni ni tabia ya mtu mwenyewe, hata akifanya kazi benki.

Baadaye alizimeza hasira zake na kujibu kwa akili.

"Nilishauriwa na rafiki yangu aliyenikaribisha nyumbani kwake. Na mimi nikuulize?" Tedi naye alimgeuzia kibao. Hii ni baada ya kumaliza kula.

"Niulize tu." Alisema huku akijilaza kitandani.

"Kwa nini umeniuliza maswali hayo?"

"Nimekuuliza kwa sababu wewe ni msichana mzuri sana. Si rahisi sana msichana kama wewe kufanya kazi kama ile. Kuna kitu gani unakitafuta au unakiwinda?"

Ni swali ambalo liligeuza hali ya hewa. Tedi aliangua kilio. Kilio kilichomshangaza Tom. Aliinua na kukaa kitandani. Alikilaza kichwa cha Tedi kwenye miguu yake na kumbembeleza.

"Samahani mpenzi kama nimekuudhi."

Zilipita dakika tano, ndipo Tedi alipoinua mdomo wake "Mpenzi hujafanya kosa kuniuliza swali hilo. Wala hakuna haja ya msamaha. Ila ni kwamba sijawahi kuulizwa swali hili na mtu yoyote. Sijawahi hata kupewa thamani hii ya kubembelezwa na wewe hapa. Kilio changu kimebeba machungu mengi sana. Ni kweli mimi siyo msichana na kuuza baa. Nafanya hivi kwa malengo tu, lakini kwa jinsi ilivyo sijui kama nitayafikia." Alisema na kuanza kulia tena.

"Usilie Tedi, hebu niambie. Inawezekana kabisa naweza kukusaidia."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**




# POGBA akataa mkataba Man United

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United itaangalia kumuuza Paul Pogba kipindi hiki cha majira ya joto baada ya Mfaransa huyo kukataa ofa ya mkataba mpya wenye thamani ya pauni milioni 50.

Majaliwa ya Pogba yamekuwa shakani tangu alipojiunga tena na United mwaka 2016, huku Real Madrid ikiendelea kuonesha nia ya kutaka kumsajili kiungo huyo.

Huku akiwa amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa, United walikuwa wana matumaini ya kumwongezea mkataba Pogba ili kuepuka kumpoteza akiwa mchezaji huru.

Lakini gazeti la Mirror limeripoti kwamba, Man United wanaangalia uwezekano wa kumuuza kipindi hiki cha majira ya joto baada ya kukataa ofa ya mkataba wa kulipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.

Habari za Pogba zimeiibua Paris Saint-Germain, huku mabingwa hao wa Ligue 1 wakiwa tayari kutoa ofa ya pauni milioni 45, ikiwa pungufu ya pauni milioni 5 kwa ofa iliyotolewa na miamba hao wa Ligi Kuu England yenye thamani ya pauni milioni 50.

Wakati kiasi cha kumuuza Pogba kikiwa kidogo ikilinganishwa na kile cha pauni milioni 89 walichokitoa mashetani wekundu hao miaka mitano iliyopita wakati wanamsajili, inaonekana wazi kwamba, hawataweza kumbakiza mshindi huyo wa kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 2018.

Real Madrid nao wapo makini kufuatilia hali ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 ili wamsajili kipindi hiki cha majira ya joto.

## MBAPPE KUJIUNGA MADRID MSIMU UJAO



**MADRID, Hispania**

KYLIAN Mbappe ameamua kutoongeza mkataba mpya na Paris Saint-Germain ili ajiunge na Real Madrid akiwa mchezaji huru msimu ujao.

Majaliwa ya Mbappe hapo kwenye viunga vya jiji la Paris yamekuwa kwenye sintofahamu baada ya kuhusishwa na uvumi wa miezi kadhaa ya kutaka kuondoka klabuni hapo.

Real Madrid na Liverpool zimekuwa zikiripotiwa kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ingawa matatizo ya kifedha yaliyotokana na mlipuko wa virusi vya corona yameziathiri klabu hizo.

Real watashindwa kumsajili Mbappe kipindi hiki cha majira ya joto, lakini gazeti la Marca limedai kwamba, hawatasubiri kwa muda mrefu kupata saini ya Mfaransa huyo.

Mpango wao wa sasa ni kusubiri Mbappe amalize mkataba wake na PSG, ili aweze kumsajili akiwa huru msimu ujao.

Ripoti hiyo imebainisha kwamba, Mbappe hana mpango wa kuhamia Liverpool, ikiwa na maana kwamba, Jurgen Klopp atatakiwa kuangalia sehemu nyingine kwa ajili ya kusajili wachezaji wa safu ya ushambuliaji.

Real Madrid sasa watalazimika kusubiri hadi kipindi cha majira ya joto kijacho kwa ajili ya kupata saini ya nyota huyo.

# Son asaini mkataba mpya Spurs

**LONDON, England**

SON Heung-min amekubali kubakia Tottenham Hotspur, huku nyota huyo wa Korea Kusini akisaini mkataba wa miaka minne utakaomuweka klabuni hapo hadi mwaka 2025.

Son alijiunga na Spurs akitokea Bayer Leverkusen mwaka 2015 na amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa mafowadi bora wa Ligi Kuu England, akifunga mabao 107 na kutoa pasi za mwisho 64 kwenye mechi 280 alizocheza katika mashindano yote.

Alikuwa mchezaji nguzo chini ya makocha mawili, Mauricio Pochettino na Jose Mourinho na mkataba wake wa sasa ulikuwa unamalizika mwaka 2023.

Hata hivyo, Tottenham wamefanikiwa kumshawishi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye sasa atakuwa chini ya kocha mpya, Nuno Espirito Santo.

Son amesema: "Tayari ilikuwa heshima kubwa kucheza hapa kwa miaka sita, klabu imeonesha heshima kubwa kwangu na nina furaha kubwa kuwa hapa.

"Naona kama nipo nyumbani kwa mashabiki wanaonizunguka, wachezaji wenzangu na benchi lote la ufundi.

"Hakukuwa na uamuzi. Lilikuwa jambo rahisi. Nina furaha kuwa hapa na ninafurahi zaidi kuendelea kucheza hapa."



HABARI MICHEZO



# BAYERN
## kuchangia walioathirika na mafuriko

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich itatoa kiasi cha euro milioni moja kwa ajili ya kuwasaidia waathirika wa mafuriko yaliyotokea wiki iliyopita nchini Ujerumani kwa kucheza mchezo wa hisani dhidi ya Schalke.

Sehemu za Ujerumani na Ubelgiji ziliathiriwa sana na mafuriko hayo yaliyogharimu maisha ya watu wengi.

Zaidi ya watu 100 bado hawajulikani waliko, huku Ujerumani ikiripotiwa vifo vya watu 177, huku maelfu wakiwa hawana makazi.

Sehemu mbili ndio zilizoathirika zaidi ambapo ni North Rhine-Westphalia na Rhineland-Palatinate, wakati kimbunga kimelikumba eneo kubwa la Bavaria.

Hivyo, Bayern imepanga kutoa kiasi cha euro milioni 1.1, huku euro milioni 1 ikigawanywa kati ya majimbo hayo ya Magharibi na euro 100,000 zitakwenda kusaidia uharibifu kusini.

Mabingwa hao wa Bundesliga pia wamepanga kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Schalke, ambao wanatokeo North Rhine-Westphalia jiji la Gelsenkirchen.

Schalke walishuka daraja msimu uliopita, ingawa tarehe ya mchezo huo utakaopigwa uwanja wa Veltins Arena bado haijatajwa.

# GRIEZMANN HATASAMEHEWA NA MASHABIKI - RAIS

**MADRID, Hispania**

MASHABIKI wa Atletico Madrid hawatamsamehe Antoine Griezmann kwa uhamisho wake wa kwenda Barcelona mwaka 2019 hata kama anataka kurudi kwa Los Colchoneros hao, kwa mujibu wa rais wa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, Enrique Cerezo.

Griezmann amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Atletico kipindi hiki cha dirisha la uhamisho wa majira ya joto, dili litakalomhusisha Saul Niguez kwenda Camp Nou.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Griezmann alifunga mabao 94 ya LaLiga kwa Atleti kwa kipindi cha misimu mitano na klabu hiyo kabla ya kujiunga na Barca miaka miwili iliyopita.

Cerezo hakukataa uwezekano wa uhamisho wa Griezmann, lakini bosi huyo wa Atleti haamini kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 atapokelewa kwa furaha na mashabiki.

Alipoulizwa kama kuna maendeleo yoyote juu ya uhamisho wa Griezmann, Cerezo alisema: "Huzungumzi kwa mtu husika."

Na alipoulizwa kama mashabiki watamsamehe Griezmann kwa kujiunga na Barcelona, Cerezo alijibu: "Sidhani."

Griezmann alikuwa na wakati mgumu kwenye msimu wake wa kwanza kule Barca akisumbuliwa na majeruhi pamoja na kushuka kwa kiwango, ingawa alifanikiwa kufunga mabao 20 kwenye mashindano yote msimu wa 2020-21 akimaliza nafasi ya pili nyuma ya Lionel Messi.



# JUVENTUS WAKARIBIA KUMSAJILI LOCATELLI

**TURIN, Italia**



JUVENTUS wanakaribia kumsajili kiungo wa Sassuolo na nyota wa michuano ya Euro 2020, Manuel Locatelli, baada ya kuwazidi miamba wa Ligi Kuu ya England, Arsenal katika mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Locatelli alianza kucheza soka na AC Milan lakini alikuwa na wakati wa kuvutia zaidi kule Sassuolo tangu alipojiunga nao na akawa nyota kwenye Euro 2020 wakati alipong'ara kwenye mechi mbili za makundi za Italia akicheza nafasi ya Marco Verratti, ambaye alikuwa majeruhi.

Arsenal waliripotiwa kuwania saini ya Locatelli wakati akiwa kwenye harakati za kuimarisha kikosi chao, lakini tyari wamemnasa Albert Sambi Lokonga.

Washikabunduki hao walikuwa tayari kufikia ada inayotakiwa na Sassuolo ya euro milioni 40 kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo, lakini sasa inaonekana wazi watamkosa.

Hata hivyo, mchezaji mwenyewe ameonesha nia ya kutaka zaidi kujiunga na Juventus badala ya Arsenal na sasa kibibi kizee hicho cha Turin kinakaribia kupata saini yake.

Juve awali ilikubali kumsajili kwa mkopo kwa masharti ya kumsajili moja kwa moja kipindi cha majira ya joto yajayo kwa euro milioni 30, lakini Sassuolo wanataka kiasi cha euro milioni 40 ili wamuuze moja kwa moja.

## KWA UFUPI

### CITY KUUZA NYOTA
MANCHESTER City wako tayari kumtoa mmoja wa wachezaji nyota akiwamo mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24, nahodha wa Algeria, Riyad Mahrez mwenye miaka 30, kiungo wa Ureno, Bernardo Silva mwenye miaka 26, au mshambuliaji wa England, Raheem Sterling mwenye miaka 26, kama sehemu ya mpango wa kuishawishi Tottenham Hotspur kuwauzia nahodha wao, Harry Kane. ***(FourFourTwo)***

### KANE PAUNI 400,000
HARRY Kane atapokea kitita cha pauni 400,000 kwa wiki atakapojiunga na Manchester City baada ya mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy, kuidhinisha kuondoka kwake wiki iliyopita. ***(Sun)***

### MBAPPE AKATAA MKATABA
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 22, hatakubali mkataba mpya Paris St-Germain, kwani anajiandaa kuhamia Real Madrid, licha ya klabu hiyo ya Ufaransa kutaka kumuunganisha na mchezaji mwenzake wa kimataifa, Paul Pogba. ***(Marca)***

### POGBA HATOSAINI
PAUL Pogba anatarajiwa kuondoka Manchester United msimu huu wa joto baada ya kukataa kusaini mkataba mpya, kwani anataka akamilishe mkataba wake wa sasa na kuondoka mwaka 2022. ***(Mirror)***

### MAN WAKOMAA NA VARANE
MANCHESTERR United pia wanang'ang'ania kufikia makubaliana na Real Madrid kumsajili beki wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28. Klabu hiyo ya LaLiga inataka kulipwa pauni milioni 50 ili kumuachilia mlinzi huyo, huku United wakiwa tayari kulipa pauni milioni 40. ***(Mirror)***

### LIVERPOOL YAMTAKA KASSIE
LIVERPOOL ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ulaya zinazotafakari uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa AC Milan na timu ya taifa ya Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 24. ***(Gazzetta dello Sport)***

### LEMINA ATAKIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE wana imani ya kumpata kiungo wa kati wa Southampton na Gabon, Mario Lemina mwenye umri wa miaka 27, baada ya kufanya mazungumzo na wachezaji kadhaa wa safu ya kati ambao bei yao iko nje ya viwango vya mshahara wa klabu hiyo. ***(Northern Echo)***


### HAZARD KURUDI CHELSEA
EDEN Hazard mwenye umri wa miaka 30, tayari ameonesha wazi hisia zake za kutaka kurejea Chelsea, baada ya vyombo vya habari vya Hispania kuripoti kuwa Real Madrid inatafuta njia ya kumuuza. ***(Mirror)***

### DAU LA RAMSDALE
ARSENAL imeambiwa na Sheffield United kuongeza ofa ya kumnunua Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 32, hadi kufikia pauni milioni 32, baada ya kukataa mara mbili dau la kumuuza kipa huyo. ***(Times)***

### ROMERO ATAKIWA CHELSEA
CHESLEA wanamtaka kipa Sergio Romero mwenye umri wa miaka 34, baada ya mkataba wake na Manchester United kukamilika. ***(Telegraph)***

### XHAKA HUYO ROMA
KIUNGO wa kati wa Arsenal, Granit Xhaka, anakaribia kukamilisha uhamisho wake kwenda AS Roma. ***(Daily Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HARY KANE RASMI KUTUA MAN CITY

**Mwenyekiti Levy akubali kuchukua pauni Mil. 160, yeye akipewa mshahara...**

**LONDON, ENGLAND**

HARY Kane ameripotiwa kukubali dili la kulipwa mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki na Manchester City baada ya mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy kukubali yaishe na kumruhusu kujiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England, EPL.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa mara ya kwanza alidokeza mpango wake wa kutaka kuondoka Spurs Mei, mwaka huu, kabla ya kujiunga na kikosi cha timu ya taifa ya England kwa ajili ya michuano ya Euro 2020.

Ofa ya kwanza ya Man City ya pauni milioni 100 kwa ajili ya kumsajili Kane ilikataliwa na klabu hiyo ya London kaskazini, kwani Levy alitaka mchezaji huyo aende nje ya ligi hiyo.

Wachezaji wenzake na Kane kwenye kikosi cha England waliripotiwa kudai kwamba, mshambuliaji huyo anaweza kukataa kujiunga na kambi ya mazoezi ya maandalizi ya msimu mpya na Tottenham ili kulazimisha kuondoka hapo Etihad.

Na sasa baada ya kushika nafasi ya pili kwenye michuano ya Euro 2020, Kane yupo tayari kujiunga na Man City.

Hata hivyo, kwa mujibu wa The Sun, hakuna haja tena kwa Kane kugomea mazoezi baada ya Tottenham kuamua kulegeza msimamo wao.

Imedaiwa kuwa fowadi huyo sasa anatarajia kukamilisha uhamisho wa kwenda katika kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola ambapo ada yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 160.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Levy amemtaarifu Kane kuhusu kubadilisha kwa msimamo wake na kwamba sasa yupo tayari kumuachia aondoke.

Kane - ambaye alifunga mabao 23 na pasi za mabao 14 kwenye Ligi Kuu ya England msimu uliopita - anatarajia kusaini mkataba wa miaka minne au mitano na mabingwa hao wa EPL.

Mshindi huyo wa kiatu cha dhahabu kwenye michuano ya kombe la Dunia mwaka 2018, anatarajia kwenda kuziba pengo lililoachwa wazi na Sergio Aguero, ambaye alimaliza muda wake wa kukaa hapo kwa muongo mmoja na kujiunga na Barcelona kipindi hiki cha majira ya joto akiwa mchezaji huru.

# AZAM YAJIPANGA KUFANYA MAKUBWA MICHUANO CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukamilisha usajili wa wachezaji wanne wapya, mabosi wa Azam FC wamesema lengo la kuboresha kikosi chao ni mahitaji ya kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya kimataifa.

Azam FC ambayo imemaliza msimu uliopita katika nafasi ya tatu, nyuma ya mabingwa Simba na Yanga iliyoshika nafasi ya pili, ni moja kati ya timu nne za Tanzania zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema wanataka kuona msimu ujao wanafanya vyema na kuendeleza mazuri yaliyofanywa na Simba katika michuano ya kimataifa msimu uliomalizika.

Alisema Simba walipambana hadi kufikia hatua ya robo fainali, hivyo msimu ujao watakiwa kuunganisha nguvu kufika mbali zaidi na hivyo Tanzania kupata heshima.

Alisema bado hawajamaliza mchakato huo wa kukijenga kikosi chao kwa sababu wanafahamu ushindani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa msimu ujao itaongezeka kutokana na kila timu haitaki kuwa wasindikizaji.

Nyota wapya ambao tayari Azam FC imeshawasajili ni pamoja na mshambuliaji wa Gor Mahia ya Kenya, Kenneth Muguna, kiungo mshambuliaji Mzambia, Charles Zulu akitokea Cape Town City ya Afrika Kusini na straika wa Timu ya Taifa ya Zambia, Rodgers Kola ambaye amemaliza mkataba wa kuitumikia Zanaco.

Kwa upande wa hapa nchini, matajiri hao wa Chamazi wamekamilisha usajili wa beki wa kushoto, Edward Charles Manyama kutoka Ruvu Shooting ya Mlandizi mkoani Pwani.



Wachezaji wa timu ya Fedha FC, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Hospitali ya Kivule jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA; JUMANNE JUMA**

## Zashushwa madaraja Zanzibar kwa kupanga matokeo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

CHAMA cha Soka Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja (UWERFA) kimezishusha daraja timu nne za daraja la pili Mkoa huo, kwa kupanga matokeo ya michezo ya mwisho ya hatua ya nne bora.

Timu hizo ni Muungano Ranger, Kundemba, Umoja wa Mbuzini pamoja na New City ambapo zilifunga magoli mengi ambayo sio kawaida katika mchezo wa Soka.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Kaimu Mwenyekiti wa chaa cha soka cha Mkoa huo, Mohmmed Ali, alisema timu hizo zimeshushwa madaraja mawili na msimu ujao zitacheza ligi daraja la nne katika Wilaya zao.

Alisema mbali na kushushwa daraja timu hizo zimepigwa faini ya Sh. 1,000,000 kwa kila timu, pamoja na Sh. 200,000 kwa kila mchezaji na viongozi ambao waliandikwa katika fomu ya uwanjani siku ya mchezo.

Alisema mbali na faini za wachezaji, chama hicho kimewafungia wachezaji wa timu zote nne na viongozi wao kwa kutojishughulisha na shughuli zozote za soka katika kipindi cha mwaka mmoja.

Alisema kitendo kilichofanywa na timu hizo cha upangaji wa matokeo kimetia doa soka la Zanzibar na sio ligi ya mkoa pekee na kuuita ni utovu wa nidhamu uliopitiliza.

## Stars U-20 kuivaa Uganda leo

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania chini ya umri wa miaka 23 (U-23), inashuka dimbani leo kuivaa Uganda katika mchezo wa pili wa mashindano ya kombe la CECAFA kwa umri huo yanayoendelea nchini Ethiopia.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kim Poulsen, alisema amejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo na kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika michezo yote ya hatua ya makundi.

Alisema licha ya kutokuwa na maandalizi ya mapema, lakini wachezaji wamefanya vizuri katika mchezo wa kwanza wa hatua hiyo ya makundi kwa kuwafunga Jamhuari ya Kidemokrasia ya Congo.

Alisema tayari amefanyia kazi upungufu uliojitokeza katika mchezo wa kwanza na sasa kikosi kipo fiti kwa ajili ya mchezo wao huo dhidi ya Uganda.

Tanzania imepangwa kundi A pamoja na timu kutoka Uganda, Kenya na DR Congo.

Katika mchezo wa kwanza, Tanzania ilipata ushindi wa 1-0 dhidi ya DR Congo), bao hilo pekee likifungwa na mshambuliaji wa Namungo FC, Relliant Lusajo dakika ya 66.

## Special Band yaahirisha uzinduzi

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI wa muziki wa dansi, Mwinjuma Muumin, amesema, uzinduzi wa bendi yake iitwayo Special Band, uliopangwa kufanyika Septemba mwaka huu, umeahirishwa hadi hapo baadaye.

Akizungumza na gazeti hili, Muumin alisema uzinduzi huo umeahirishwa kutokana na sababu zilizo juu ya uwezo wa uongozi wa bendi hiyo na hivyo wanamuziki wanaendelea kujipanga zaidi.

"Tulipanga kuzindua rasmi bendi yake mwezi Septemba na kisha Desemba tungezindua albamu mbili kwa mpigo, lakini zimejitokeza sababu ambazo ziko juu ya uwezo wetu, hivyo tumeahirisha," alisema Muumin.

Alisema, tangu Januari mwaka huu, bendi hiyo ilikuwa ikiandaa wimbo mmoja kila mwezi na kufankiwa kukamilisha nyimbo sita zikiwamo za 'Yatima Mzee, Mwanangu, Fenesi' na 'Kwa Mparange Sihami'.

"Mwanzoni mwa Juni mwaka huu tulitambulisha wimbo wa Mkonga wa Tembo kwenye onyesho letu tulilolipa jina la White Part na sasa kilichobaki ni kusonga mbele ni harakati za kurejesha heshima ya dansi nchini," alisema.

Aidha, Muumin alisema, katika moja ya mikakati yake ni kushirikisha wasanii mbalimbali wa muziki wa kizazi kipya wa ndani na nje ya nchi, kwenye baadhi ya nyimbo za bendi hiyo ili kupata vionjo tofauti.

"Ninatamani kumshirikisha msanii wa muziki wa kizazi kipya kama Jose Chamilione wa Uganda katika nyimbo zetu za baadaye na wengine wa Tanzania kama Zuchu, Nandy na wengine," alisema.

# Michezo



Jumamosi Julai 24, 2021

Nipashe

## Kane rasmi kutua Man City

HABARI UK. 22



Wachezaji wa Yanga, Juma Makapu ( kushoto), na Tuisila Kisinda wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Chuo cha Hali ya Hewa mkoani Kigoma kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya fainali ya FA dhidi ya Simba itakayochezwa kesho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Coastal, Mtibwa kubaki Ligi Kuu leo?

**Na Adam Fungamwango**

TIMU mbili zitakazocheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao zitajulikana rasmi leo wakati mechi za marudiano za mchujo zitakapopigwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga na Jamhuri Morogoro.

Coastal Union, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 1988 baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 Jumatano iliyopita dhidi ya Mabingwa wa Ligi Kuu ya Muungano mwaka 1990, Pamba ikiwa ugenini, Uwanja wa Nyamagana mjini Mwanza, leo itakuwa na kazi moja tu ya kuhakikisha inasalia kwenye Ligi Kuu kwa kupata ushindi.

Baada ya ushindi wa mabao 4-1, Mtibwa Sugar ambayo inaonekana tayari ni kama imeshabaki kwenye Ligi Kuu, itakuwa nyumbani kurudiana na Transit Camp, mara baada ya mechi iliyochezwa Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Coastal Union amesema mechi itakuwa ngumu kwa sababu Pamba ni timu nzuri, lakini wao wamejiandaa vema.

"Kuna makosa tuliyafanya, lakini tumeyarekebisha." Alisema.

Coastal Union na Mtibwa Sugar zinacheza mechi za mchujo maarufu kama 'play off', baada ya kushika nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, zikiepuka kushuka daraja moja kwa moja, huku Pamba, Transit Camp, zikitoka kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Pamba iliyoshuka kwenye miaka ya mwanzoni imekuwa kwenye majaribio kadhaa ya kutaka kurejea, lakini imekuwa ngumu kwao, kwani msimu wa 2018/19, ilikaribia kufanya hivyo, lakini ikafungwa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye mechi ya 'play off' ugenini, baada ya suluhu nyumbani.

# GOMES: TUMEKUJA KUFUNGA HESABU

### ●●● Yanga yenyewe yasema Simba hawataamini kitakachowakuta kwa sababu...

**Na Somoe Ng'itu, KIGOMA**

HAWATOKI! Hayo ni maneno yanayosemwa na kila upande kuelekea mchezo wa fainali ya Kombe la FA utakaowakutanisha watani wa jadi, Simba na Yanga wote kutoka jijini Dar es Salam utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema kikosi chake kinaupa umuhimu mkubwa mchezo wa kesho na kila mchezaji yuko tayari kupambana kusaka matokeo mazuri.

Gomes alisema wamejiandaa vyema kuhakikisha wanakamilisha 'hesabu' kwa kuchukua ubingwa wa michuano hii kwa mara nyingine kama walivyofanya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema wachezaji wote walioko mkoani hapa wako katika hali nzuri na wanachosubiri ni muda wa mchezo ufike ili wakamilishe majakumu yaliyowaleta mkoani hapa.

"Tunafurahi kila kitu kiko sawa, tunataka kushinda makombe yote ya ndani, ingawa tunajua mchezo utakuwa mgumu na wenye ushindani," alisema Gomes.

Aliongeza wanahitaji kucheza kwa kiwango cha juu ili wawapatie furaha watu wote muhimu wanaowajali.

" Ushindi kwetu ni muhimu sana, tutapambana kusaka ushindi kwa ajili ya makundi matatu, kwanza kwa ajili ya Mo (Mwekezaji-Mohammed Dewji), Barbara (Gonzalez) na mashabiki wetu ambao ni muhimu zaidi, wamekuwa wakitusapoti lila siku, hatutaki kuwaangusha," Gomes aliongeza.

Mratibu wa Simba, Abbas Ally aliliambia gazeti hili kila kitu kinakwenda vizuri katika kambi yao baada ya kumaliza mazoezi jana mchana wanatarajia kufanya mazoezi ya mwisho leo asubuhi.

"Tuko vizuri, tunaamini tutakifuata kile tulichokifuata Kigoma, tulianza kutetea ubingwa wa Ligi Kuu, sasa tunaenda kumalizia na FA," alitamba mratibu huyo.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na kilichobakia kwao ni kwenda kupambana kwa ajili ya kushinda mechi hiyo ya kufunga msimu wa 2020/21.

Mfikirwa alisema kikosi chake hakina wasiwasi lakini kimedhamiria kushinda kombe la michuano hiyo kama walivyodhamiria.

"Sisi ndio mabingwa wa FA, ni suala la muda tu linasubiriwa," alisema kwa kifupi kiongozi huyo.

Kikosi cha Yanga jana asubuhi kilifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Chuo cha Hali ya Hewa mkoani hapa na baada ya kumaliza programu hiyo, msafara wa magari mbalimbali ulikisindikiza kurejea hotelini.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema maandalizi yote muhimu kuelekea fainali hiyo yamekamilika na wanawataka mashabiki mbalimbali waliokata tiketi kujitahidi kuingia uwanjani mapema ili kuepuka usumbufu.

Ndimbo alisema waamuzi wa mchezo huo wakiongozwa na Ahmed Arajiga kutoka Manyara wameshawasili Kigoma tangu jana na mchezo huo utafanyika kuanzia saa 10:00 jioni kama ilivyotangazwa.

Simba ndio bingwa mtetezi wa mashindano hayo ambayo hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Wakati huo huo Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, amewataka mashabiki wote wa soka watakaoingia kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika kufuata tahadhari zote zinazohusiana na ugonjwa wa Corona.

Andengenye alisema ni vyema mashabiki wakafika uwanjani hapo wakiwa wamevaa barakoa ili kujiweka salama na kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa huo.

Kiongozi huyo aliwakaribisha wageni wote waliofika mkoani hapa kwa ajili ya kuangalia mchezo huo na kuwahakikishia ulinzi na usalama utakuwa wa kiwango cha juu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002